



Vodacom Tanzania Public Limited Company

Taarifa ya Pamoja ya Mwaka

kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024

Pamoja tunaweza



Yaliyomo

Utangulizi

Sisi ni nani
Vodacom Tanzania kwa ufupi
Taarifa ya Mwenyekiti
Thamani tuliyojenga

Biashara yetu

Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu
Bidhaa na huduma zetu

Azma yetu

Kuiwezesha jamii
Kuilinda sayari

Ufanisi wetu kifedha

Taarifa ya Mkurugenzi wa Fedha

Utawala

02	Viongozi wetu	22
03	Taarifa ya uongozi wa kampuni	26
04	Taarifa ya shughuli za uongozi	28
06	Taarifa ya masuala ya ujira 2024	30

Taarifa ya Mkutano Mkuu

08	Fomu ya Mwakilishi	37
10	Maelekezo ya fomu ya mwakilishi	38

Taarifa za ziada

13	Taarifa kuhusu umiliki	39
15	Taarifa za kampuni	40
	Dai la haki	41

16



Taarifa ya mwaka 2024 ya Vodacom Tanzania

Hii ni taarifa ya nane ya mwaka ya Vodacom Tanzania, na ya saba tangu kampuni iorodheshwe kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam tarehe 15 Agosti 2017.

Taarifa hii ambayo inawalenga wawekezaji wetu wa sasa na pia wa siku zijazo, inatoa maelezo ya jumla ya biashara yetu, muundo wa biashara, mazingira ya uendeshaji, kupitia mikakati yetu, mafanikio ya mfumo wa undeshaji na utawala kwa mwaka wa fedha ulioanzia tarehe 1 Aprili 2023 hadi 31 Machi 2024. Utaratibu wetu wa kutoa taarifa ya mwaka umekuwa ukiongozwa na kanuni na masharti yaliyo katika Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha (IFRS), Kanuni za Soko la Hisa la Dar es Salaam za mwaka 2022 na Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Mkaguzi huru, Ernst & Young ('EY') amethibitisha taarifa zetu za fedha za mwaka na kutoa hati safi. (ukurasa wa 77 hadi 79 kwenye nakala ya kiingereza).

Bodi imeshiriki kikamilifu katika uandaaji na uwasilishaji wa taarifa hii. Na tunaamini kuwa taarifa hii inaelezea masuala yote muhimu, na inawasilisha maelezo yenye usahihi kuhusu utendaji wa kundi la Makampuni kwa kipindi husika na vilevile inatoa taswira halisi ya mikakati yetu ya utekelezaji. Wakurugenzi wanaamini kuwa kutangaza mipango mkakati ya Vodacom Tanzania, hakutaleta athari yeyote ile katika medani za ushindani wa kibiashara. Bodi ilipitisha taarifa hii ya mwaka tarehe 17 Julai 2024.

Imesainiwa kwa niaba ya Bodi na:

Jaji (mstaafu) Thomas B. Mihayo
Mwenyekiti
17 Julai 2024

Philip Besiimire
Mkurugenzi Mtendaji
17 Julai 2024

Azma yetu kuu ya kuongeza thamani katika jamii

Azma kuu ya Vodacom Tanzania ni 'kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora'. Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (UN SDGs) yanatoa taswira ya muonekano wa kesho iliyo bora, kwa kuweka malengo ya muda mrefu ya kuondoa umaskini, kulinda mazingira na kuleta ustawi kwa wote ifikapo mwaka 2030. Vodacom Tanzania imejikita katika kutumia teknolojia na rasilimali zake kama kampuni ya mawasiliano inayoongoza barani Africa katika kufikia malengo haya, kuunga mkono serikali, jamii, biashara na watu binafsi katika kujenga kesho iliyo bora. Tunachangia kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa ya maendeleo kupitia biashara yetu kwa kuwezesha mawasiliano ya data, ujumbe, sauti na huduma za fedha na hivyo kutoa mchango muhimu katika kutimiza malengo ya maendeleo duniani.

Vodacom Tanzania imeainisha na kuweka kipaumbele katika malengo nane ya maendeleo endelevu ambayo tunaamini tunaweza kuwa na mchango chanya:



Utendaji wetu katika kuchangia Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu umeainishwa vizuri katika taarifa hii, na hasa katika sehemu ya Azma Yetu (ukurasa wa 12 hadi 15), pamoja na maelezo zaidi yanayopatikana katika Taarifa yetu ya ESG kupitia tovuti yetu: <https://vodacom.co.tz/financials> na katika taarifa ya ESG ya Kampuni yetu mama ya Vodacom Group <https://www.vodacom.com/integrated-reports.php>.

Ili kupata taarifa zaidi:



Soma **taarifa hii** kwa kina



Soma zaidi katika tovuti
www.vodacom.co.tz

Maelezo ya msingi

Tafadhali zingatia kwamba, hii ni tafsiri ya taarifa ya mwaka kwa ufupi. Taarifa kamili ya mwaka imetolewa kwa lugha ya kiingereza. Iwapo utatokea mkanganyiko wa tafsiri, taarifa ya kiingereza itatumika.

Sisi ni nani

Vodacom Tanzania ni kampuni inayoongoza nchini Tanzania kwa kutoa huduma za mawasiliano kwa wateja wa matumizi binafsi na biashara ikiwa ni pamoja na huduma za simu sauti, data, ujumbe mfupi wa maneno na huduma za fedha kwa wateja zaidi ya **milioni 19.6**

Vodacom Tanzania iliorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam mnamo Agosti 15, 2017. Mmiliki mkubwa wa Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu (yaani 'Kundi la Kampuni za Vodacom') ni Vodacom Group Limited, kampuni iliyosajiliwa Afrika Kusini ambayo nayo inamilikiwa na Vodafone Group PLC ya Uingereza.



Dira yetu

Tunakoelekea na tunataka kuwa nani

- Kuwa kampuni ya kidigitali inayoongoza ambayo inawezesha jamii iliyounganishwa katika mtandao
- Kuiunganisha jamii kwa kesho iliyo bora
- Kuwa mwajiri bora (mahali bora pa kufanyia kazi)

Kwa namna gani

Namna ya utekelezaji

- 1** Kuaminiwa na wateja
- 2** Kujenga mustakabali
- 3** Kufanya majaribio – kujifunza haraka
- 4** Kutekeleza mambo yote kwa pamoja

Vipaumbele vyetu kimkakati


Ukuaji kupitia biashara mpya huku tukilinda biashara zetu kuu

Kulinda kwa bidii biashara ya huduma ya mawasiliano ya simu	Kuzifikia fursa za kutoa huduma ya data majumbani na maofisini	Kukodisha sehemu ya rasilimali zetu
Kuongeza wigo na kuikuza huduma ya M-Pesa	Ubunifu na kuongoza katika huduma kwa wateja wa kibiashara	Thamani ya chapa yetu katika soko


Udigitishaji wa huduma kwa wateja **Uongozi katika teknolojia ya mtandao na TEHAMA** **Kuwaendeleza wafanyakazi na kuwa na timu ya watu wanaofanya kazi kwa ufanisi**

Kuongeza ufanisi wa matumizi ya mtaji


Vodacom Tanzania kwa ufupi




Uwekezaji kwa miaka 4 (shilingi bilioni)




Wateja wa siku 90 (milioni)



Idadi ya watu wanaofikiwa na mtandao wetu wa 3G na 4G



Idadi ya minara



Idadi ya minara ya 4G



Idadi ya watu wanaofikiwa na mtandao wetu wa 4G



Taarifa ya Mwenyekiti

Ninayo furaha kuwasilisha taarifa ya nane ya mwaka ya Vodacom Tanzania, na ya saba tangu tuorodheshwe katika Soko la Hisa la Dar es Salaam mwezi Agosti 2017. Tukiwa kampuni ya kwanza na pekee ya mawasiliano ya simu kutekeleza agizo la kisheria la Serikali la kuorodheshwa katika soko la hisa, na kuvutia wawekezaji zaidi ya 40,000 – ni ushahidi wa msimamo thabiti wa Vodacom katika utii wa sheria na taratibu, na kuchangia katika ukuaji na maendeleo ya Uchumi wa Tanzania.

Mwaka huu umekuwa mzuri sana kwa kampuni, kwa matokeo yake thabiti kifedha na kiutendaji yanayoakisi mkakati bora na utekelezaji wenye ufanisi.



Mwaka huu, faida baada kodi iliongezeka kwa **19.9%** hadi **shilingi bilioni 53.4**, ambayo itaiwezesha Bodi kupendekeza kwa wanahisa kupitisha gawio la angalau **50% ya faida baada ya makato ya kodi**, kwa mujibu wa sera yetu ya gawio.

Jaji (mstaafu) Thomas Mihayo

Licha ya ushindani mkubwa wa soko, inafurahisha kuona ongezeko la idadi ya wateja wa Vodacom katika soko na kuongoza kwa kuwa na 30.5%¹, ya soko na pia ongezeko la idadi ya wateja katika huduma za data kwa njia ya simu na M-Pesa. Idadi ya wateja wetu iliongezeka kwa 16.9% hadi kufikia wateja milioni 19.6, ukuaji uliochangia katika ongezeko kubwa la mapato yetu. Ongezeko la kuridhisha la 66% la data iliyosafirishwa kwa teknolojia ya 4G, linaakisi matokeo chanya ya upanuzi wa mtandao wetu wa data, utekelezaji madhubuti wa juhudi za kuongeza watumiaji wa simu janja, na ubora wa huduma za data kwa simu zikichagizwa na mifumo ya uchanganzuzi wa matumizi ya wateja (CVM). Ongezeko hili la matumizi ya huduma ya data kwa simu linatupa matumaini kuwa **bado kuna nafasi zaidi ya ukuaji** wa huduma hizi siku za usoni iwapo tutachochea ongezeko la utumiaji wa simu janja hapa nchini.

Mbali na utendaji thabiti kifedha wa Kampuni, inafurahisha kuona matokeo chanya ya shughuli zake katika kuhamasisha **huduma jumuiishi za kifedha na kupunguza ombwe la kidigitali**. Hili linatekelezwa kupitia huduma za kibunifu za M-Pesa, zinazolenga kuboresha huduma za kidigitali katika sekta muhimu kama vile kilimo, afya, elimu na huduma za serikali, pamoja na uwekezaji endelevu katika miundombinu ya mtandao na kuongeza upatikanaji wa vifaa janja vya gharama nafuu. Kupitia uwekezaji huu, si tu kwamba Vodacom inaimarisha ustahimilivu wake na fursa za ukuaji wa muda mrefu, bali pia inaleta fursa katika jamii na kutoa mchango muhimu katika uchumi wa Tanzania.

Uwezo wa Kampuni kufanya uwekezaji huu katika miundombinu na katika bidhaa na huduma bunifu, unachochewa na **majadiliano na mahusiano chanya kati ya serikali na jamii ya wafanyabiashara** juu ya masuala yanayohusu TEHAMA, na vilevile uimara katika udhibiti wa sekta. Mabadiliko ya hatua kwa hatua na hatimaye, kuondolewa kwa tozo kwenye huduma za kutuma na kupokea fedha kati ya wateja wetu yanaridhihirisha matokeo chanya ya majadiliano, na yameleta faida kwa pande zote na kuongeza nafasi ya TEHAMA katika kuchangia vipaumbele vya maendeleo ya nchi.

Kwa nafasi yangu ya Uenyekiti wa Bodi, **ninawajibika kuhakikisha kuwa Bodi inatekeleza kazi zake za uangalizi na usimamizi** ili kuhakikisha kuwa Kampuni inafanikisha ukuaji endelevu na mafanikio chanya kifedha kwa njia ya uwajibikaji na uadilifu huku ikizingatia maslahi bora ya wadau wake wote. Tathmini yetu huru ya hivi karibuni juu ya utendaji wa Bodi inanipa uhakika kuwa tuna kiwango cha kutosha cha ujuzi, uzoefu, utofauti wa mawazo na mitazamo miongoni mwa wakurugenzi wetu, yanayohitajika ili kudumisha utamaduni thabiti wa uwajibikaji na usimamizi huru wa mikakati na mwelekeo na utendaji wa Kampuni.

Nikiangalia siku zijazo, ni wazi kuwa migogoro inayoendelea barani Ulaya na Mashariki ya Kati pamoja na kuongezeka kwa mivutano katika ukanda wa Bahari ya China Kusini kunaweza kuathiri zaidi uchumi wa dunia ambao tayari umeathirika. Mashambulizi ya meli katika Bahari ya Shamu hayajavuruga tu njia muhimu zaidi ya usafiri wa meli, bali pia yaliharibu nyaya zetu za mawasiliano zinazopita chini ya Bahari hapo mwanzoni mwa mwezi Machi. Hali hii inadhihirisha vihatirishi vinavyoweza kutokea katika huu uchumi wa dunia uliyoungana pamoja. Pia kuna mashaka kuhusiana na matokeo ya chaguzi mbalimbali zinazofanyika mwaka huu – ukiwemo uchaguzi wa Marekani, India, Umoja wa Ulaya, Uingereza na Afrika Kusini – ambayo yanaweza kupelekea mabadiliko mbalimbali ya taratibu za kibiashara duniani na kikanda.

Licha ya mazingira haya ya mashaka ya kisiasa duniani na vilevile changamoto za ndani kama vile upatikanaji wa fedha za kigeni, bado nina matumaini na hali nzuri ya uchumi wa nchi na ukuaji endelevu wa Vodacom. Nina uhakika kuwa Kampuni ina mkakati sahihi, timu ya uongozi thabiti na uwezo wa ubunifu wa huduma vinavyoiwezesha kampuni kukabiliana na changamoto mbalimbali na kuendelea ukuaji wa muda mrefu. Tunatambua kwamba mafanikio tuliyoypata mpaka sasa hayapaswi kutufanya tujisahau bali tuongeze juhudi zaidi, hasa kwa kuzingatia ushindani katika soko na mabadiliko ya mahitaji ya wateja wetu.

Ninapenda kuwashukuru wenzangu katika Bodi kwa kuendelea kutimiza vyema wajibu wao, na kwa niaba yao, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa timu ya viongozi waendeshaji wa Vodacom, wafanyakazi na washirika wote kibiashara kwa mchango wao uliopheleka matokeo mazuri kiutendaji. Mwishoni, kwa mara nyingine ninapenda kuwaomba ninyi wadau wetu muisome taarifa hii ya mwaka na kuchangia mawazo yenu kuhusu utendaji wa Kampuni na mkakati wake. Kuiwajibisha Kampuni kiutendaji na kutoa taarifa ni muhimu katika kutusaidia sisi sote kutekeleza azma ya Vodacom ya kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora.




Jaji (mstaafu) Thomas Mihayo
Mwenyekiti
17 Julai 2024

1. Kwa mujibu wa takwimu za mawasiliano za robo mwaka za Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania za Machi 31, 2024.

Thamani tuliyojenga

Ufanisi wetu



Kwa wateja wetu

Utoaji wa huduma muhimu za mawasiliano

Kuongeza na kuwezesha huduma jumuishi za kifedha kupitia huduma katika M-Pesa

Tumeendelea na huduma zetu jumuishi ili kuhudumia wateja wenye mahitaji maalum

Uongozi katika kipimo cha kuridhika kwa wateja (NPS)

Tumeendelea kupanua wigo wa mtandao wetu

Wigo wa teknolojia ya 4G²

66.1%

ya idadi ya watu (ongezeko la alama za asilimia 4.8)

Wigo wa teknolojia ya 3G³

76.5%

ya idadi ya watu

Wigo wa teknolojia ya 2G

94.6%

ya idadi ya watu (ongezeko la alama za asilimia 0.9)



Ujumuishi kidijitali kupitia upanuzi wa mtandao kwa kutumia uwekezaji tulioufanya mwaka huu

1. Ukiiondoa matumizi katika kuunganisha na ununuzi – ununuzi wa Smile Telecommunications Tanzania Limited.

2. Imepimwa katika kiwango cha 1 mbps (nje).

3. Imepimwa kwa kiwango cha 1 mbps (nje). Takwimu za wigo zilazoripotiwa katika miaka iliyopita zilikuwa zinahusiana na wigo katika mtandao wa 3G.



Kwa wanahisa wetu

Shilingi bilioni 26.7

zimependekezwa kuwa gawio kwa wanahisa

Jumla ya

Shilingi bilioni 571

zimekipwa kama gawio tangu Kampuni iorodheshwe kwenye soko la hisa mwaka 2017



Kwa wafanyakazi wetu

Shilingi bilioni 75

zimetumika kwa ajili ya wafanyakazi, ikiwemo mishahara, mafunzo na kuendeleza ujuzi

Tumetoa mafunzo ya kujiendeleza kwa njia ya mtandao kwa zaidi ya wafanyakazi

600

Uwakilishi wa

46.7%

wa wanawake kwenye uongozi



Katika jamii yetu

Tumechangia jumla ya

Shilingi bilioni 523

kwenye fedha za umma kwa njia ya kodi na tozo, masafa na tozo za mamlaka za uhabiti wa sekta

Tumeunga mkono programu za Serikali kufikisha mawasiliano vijijini kwa kujenga

minara 313

katika kipindi cha cha zaidi ya miaka kumi ya ushirikiano

Kuchochea kilimo – zaidi ya

shilingi bilioni 16

zimekipwa kwa wakulima waliojisajili katika mfumo wa M-Kulima

Programu

yetu ya kuokoa maisha ya

m-mama

sasa inapatikana katika mikoa yote Tanzania

Shilingi bilioni 630.0

zimetumika kwa ajili ya malipo ya bidhaa na huduma za wasambazaji wa ndani na makampuni washirika takriban 300 nchini Tanzania

Takriban

Shilingi bilioni 6

zimetumika katika uwekezaji kwenye jamii¹

Takribani ajira

200 000²

zisizo za moja kwa moja zimetolewa kwa waTanzania



1. Inajumuisha ufadhili wa fedha na thamani ya vifaa au vitu vilivyotolewa kupitia matukio mbalimbali ya Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR).
2. Inajumuisha wafanyabiashara wadogo huria (Freelancers) na mawakala wa M-Pesa.

Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu



Huu umekuwa mwaka wa kipekee kwetu uliokuwa na ufanisi mkubwa kifedha na muendeleo wa mchango wetu katika kuhamasisha maendeleo jumuishi ya kiuchumi na kupunguza ombwe la kidigitali nchini Tanzania. Utendaji wetu huu wa kuridhisha unaakisi uthabiti na utekelezaji makini wa mkakati wetu, na vilevile mazingira wezeshi kiudhibiti na kisera.

M-Pesa imepiga hatua muhimu kwa kuvuka idadi ya wateja milioni 10.

Philip Besiimire

Biashara yetu ya mawasiliano kwa simu ilizidi kuimarika na kupelekea ongezeko la mapato ya huduma kwa 19.4% hadi kufikia shilingi trilioni 1.3. Pia, tulijiimarisha katika nafasi yetu ya uongozi katika soko tukiwa tunashikilia 30.5%¹ ya wateja wote wa soko. Utendaji huu wa kuridhisha ulichangiwa na malengo yetu ya makusudi ya kuongeza wateja. Ni jambo la kutia moyo kuona tumemamaliza mwaka tukiwa na ongezeko la idadi ya wateja la 16.9% hadi wateja milioni 19.6, na ongezeko la 15.1% la watumiaji wa data hadi kufikia milioni 10.1 ambapo kati yao, zaidi ya 65% walikuwa watumiaji wa simu janja, hali inayotupa fursa nzuri ya kukuza biashara.

Huduma yetu ya kifedha – M-Pesa, imepiga hatua muhimu kwa kuvuka idadi ya wateja milioni 10, ongezeko la watumiaji wapa takriban milioni mbili katika mwaka huu, na kufanikiwa kumiliki 38.2%¹ ya wateja wa soko. M-Pesa inaendelea kuwa sehemu muhimu ya maisha ya kifedha ya mamilioni ya Watanzania, na kutoa mchango muhimu katika ujumuishi kifedha. M-Pesa inawezesha upatikanaji wa huduma za kisasa za fedha kwa njia ya simu ikiwemo malipo ya kidigitali, upatikanaji wa mikopo kidigitali, kuweka akiba, utoaji wa huduma za bima na mengineyo. Huduma hizi za kimageuzi zinafanya M-Pesa kuwa si tu mwezeshaji wa ujumuishi kifedha, bali pia zana ya uwezeshaji wa kiuchumi hasa kwa jamii isiyotumia huduma za benki.

M-Pesa imekuwa na ufanisi wa kipekee ikiwa na kiwango cha kuridhisha cha ukuaji mwaka hadi mwaka katika vigezo vyote vya msingi, ikiwemo ongezeko la mapato la 27.8% na ongezeko la 36% la jumla ya thamani ya miamala iliyochakatwa kupitia M-Pesa hadi kufikia thamani ya wastani wa zaidi ya shilingi trilioni 8 kwa mwezi. Huduma zetu mpya ndani ya M-Pesa² zimekuwa kichocheo katika kusukuma ukuaji na wigo wa mapato. Huduma msingi za M-Pesa kama vile kutuma na kutoa fedha, pia zilionyesha ufanisi mzuri ikichochea na ondoleo la tozo katika miamala ya kutuma na kupokea pesa kati ya wateja wetu.

Huduma zetu za data majumbani na maofisini ambazo zinatoa fursa ya ukuaji thabiti ni miongoni mwa maeneo tuliyofanya vizuri kutokana na juhudi zetu kubwa za kutoa huduma nzuri za data majumbani na maofisini. Katika mwaka huu, tulifikisha ongezeko la kuridhisha la zaidi ya 35% ya idadi ya nyumba na biashara tulizoziunganisha katika mtandao wetu.

1. Kwa mujibu wa takwimu za mawasiliano za robo mwaka za Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania za Machi 31, 2024.
2. Huduma hizi ni pamoja na mikopo ya muda mfupi, akiba, bima, uhamishaji fedha kimataifa na malipo kwa wafanyabiashara.

Tulifanya vizuri pia kwenye **huduma kwa wateja wa kibiashara**, hasa katika kuhudumia biashara ndogondogo na za kati kupitia uunganishwaji wa huduma za data. Pia tunaona fursa ya kukuza biashara kupitia mfumo wetu wa vitu vilivyounganishwa kwa intaneti (IoT), unaowezesha kutoa huduma muhimu za ufuatiliaji, kama vile matumizi ya mita janja kwa makampuni ya umeme na maji, mifumo ya ufuatiliaji katika kampuni za usafirishaji, na kilimo cha kisasa.

Kwa upande mwingine, **biashara yetu ya ukodishaji wa sehemu ya rasilimali zetu** imeendelea kuwa sehemu tunayoona fursa ya kuendeleza ukuaji wa biashara yetu. Hivi sasa tunahudumia takribani theluthi mbili ya watoa huduma ya intaneti wote (ISPs) nchini Tanzania, ambayo ni hatua inayotia moyo.

Uthabiti wa chapa yetu ya Vodacom ni taswira ya ubora wa mtandao wetu, watu wetu na huduma zetu kwa wateja, na vilevile kutambuliwa kwa mchango wetu kupitia azma na wajibu wetu kwa jamii ya, 'kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora'. Utekelezaji makini wa mkakati wetu uliwezesha na wafanyakazi wetu wenye ujuzi, ari na hamasa ya hali ya juu ambao ni miongoni mwa wafanyakazi bora kabisa katika kundi la makampuni ya Vodafone kama ilivyodhihirishwa na matokeo ya kipimo cha 'Ari ya Timu' na 'Ushirikishwaji wa Wafanyakazi'. Juhudi za nguvukazi hii yenye ubora wa hali ya juu ilituwezesha kuimarisha nafasi inayoshikiliwa na chapa yetu na kuendelea kuwa katika nafasi ya mbele katika kiwango cha kuridhika kwa wateja (NPS) katika kipindi chote cha mwaka. Inapendeza kuona, tulimaliza mwaka tukiongoza kwa alama thabiti za tarakimu mbili juu ya mshindani wetu wa karibu katika kipimo cha NPS.

Kwa kuzingatia **azma yetu ya 'Kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora'** na lengo letu la kupunguza ombwe la kidigitali Tanzania, mwaka huu tumeweza shilingi bilioni 170.1 katika kupanua wigo na uwezo wa mtandao wetu, kujenga minara ya teknolojia ya 4G na 5G, na kuendelea kuboresha miundombinu yetu ya TEHAMA ili kuendelea kuboresha huduma kwa wateja, kuimarisha usalama wa mtandao na kutuwezesha kuzifikia fursa kubwa zilizopo katika maeneo kama vile mifumo ya kisasa ya vitu vilivyounganishwa kwa Intaneti (IoT). Mnamo mwezi Machi 2024, tulimaliza kwa kiasi kikubwa taratibu za kuinunua kampuni ya Smile Communication Tanzania Limited – 'Smile'. Ununuzi huu unatuwezesha kumiliki masafa ya 20 MHz ya 800MHz na 20 MHz ya 2 600MHz, ambayo yatatuwezesha kuendelea kuimarisha miundombinu ya mtandao wetu na ubora wa huduma kwa wateja.

Uimara wa mtandao wetu umekuwa nyenzo muhimu katika utekelezaji thabiti wa azma na wajibu wetu kwa jamii. Mwaka huu tuliihuisha azma yetu kutoka nguzo tatu za "jamii ya kidigitali", "ujumuishi kwa wote" na "sayari" kwenda nguzo mbili za "kuiwezesha jamii" na "kuilinda sayari" katika zama za maisha ya kidigitali.

Azma yetu hutuwezesha kutoa mchango wa ukuaji wa jamii endelevu ya kidijitali, ambapo tumeendelea kuona matokeo chanya. Mfano mzuri wa matokeo haya ni programu ya m-mama iliyojikita katika afya ya uzazi, programu yetu ya Code Like A Girl, inayokusudia kuhamasisha ushiriki wa wasichana katika masomo ya sayansi na hesabu, mipango yetu ya kuwaendeleza wanawake katika uongozi, na harakati zetu za upandaji miti nchini. Pia, kupitia jukwaa letu la kibunifu la kilimo la M-Kulima, wakulima wadogo zaidi ya milioni 3 wameunganishwa kwenye mnyororo wa thamani wa kilimo ili kupata taarifa za kilimo na masoko kupitia aplikesheni na ujumbe mfupi "SMS", huku wakipokea malipo ya haraka na salama kupitia M-Pesa. Kwa upande mwingine, mkakati wetu unaolenga kuongeza ufanisi katika matumizi ya nishati unatusaidia kupunguza athari katika mazingira, na hivyo, kuchangia katika matarajio ya kampuni yetu mama – ya kundi la makampuni ya Vodacom, yenye malengo ya kupunguza kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa hewa ya ukaa ifikapo mwaka 2035.

Ufanisi wetu kifedha umeendelea kuwa mzuri ikiwa ni muendelezo wa uzalishaji wa faida tangu mwaka uliopita. Tulipata ongezeko la faida kabla ya kodi na uchakavu (EBITDA) la karibu 20%, lililochangia ukuaji wa faida ya uendeshaji wa 65% na faida baada ya kodi ya kiasi cha shilingi bilioni 53.4.

Matokeo haya yalichagizwa na jitihada zetu za kuokoa gharama, ambazo zilitekelezwa kwa umakini bila kuleta athari katika ubora wa huduma zetu kwa wateja au uwekezaji. Kutokana na ufanisi huu mzuri kifedha, tunaomba Bodi ipendekeze gawio sawa na 50% ya faida baada ya kodi – kwa mujibu wa sera yetu ya gawio.

Utendaji wetu imara mwaka huu ulichangiwa na **mazingira thabiti ya kisiasa na kisera**, na vilevile maendeleo chanya ya kiudhibiti, kama vile kuondolewa kwa tozo katika miamala ya kutuma na kupokea pesa kati ya wateja wetu na punguzo la tozo la usimikaji wa nyaya za mawasiliano kwenye hifadhi za barabara. Sera rafiki za serikali kwa uwekezaji, ukuaji wa sekta binafsi, na uwekezaji zaidi katika sekta ya umma, zimetutia moyo na kutupa motisha ya kupanga na kuwekeza kwa kujiamini kwa manufaa ya siku zijazo.

Tunatazamia fursa zaidi za ukuaji kibiashara huko mbeleni hasa kwa kuzingatia kuwa Tanzania ni taifa lenye vijana wengi na idadi ya watu inayoendelea kukua, pamoja na kiwango chenye nafasi ya kukua cha matumizi ya huduma za kidigitali. Kama mshiriki anayeongoza katika nafasi ya huduma za fedha za kidigitali, Vodacom ina nafasi nzuri zaidi ya kujenga thamani stahiki kwa wadau wetu wote.

Nina imani tuna mkakati sahihi, uwezo thabiti na timu makini itakayoendeleza nafasi yetu ya uongozi katika soko licha ya changamoto mbalimbali za kisiasa na kiuchumi duniani na hapa nchini kama vile kuyumba kwa viwango vya kubadilishia fedha za kigeni, ushindani katika soko na matarajio makubwa ya wateja wetu. Nafasi thabiti tuliyonayo katika soko, pamoja na bidhaa zetu na huduma bunifu, zinatuweka katika nafasi nzuri ya ukuaji endelevu kibiashara kwa muda mrefu.

Uwezo wetu wa kukuza na kuongeza thamani ya biashara yetu umeweza na mchango kutoka kwa wadau wetu wote – wateja wetu, wadhibiti, jamii, wawekezaji, washirika wetu kibiashara na wafanyakazi wetu. Ninapenda kuwashukuru nyote, kwa kuendelea kutuunga mkono na juhudi zenu katika kazi. Ninapenda kipekee kuwashukuru wenzangu katika timu ya uongozi wa Vodacom na wafanyakazi wote kwa mchango wenu katika utendaji thabiti wa Kampuni mwaka huu.

Kwa pamoja, ahadi yetu ni kuendelea kujenga thamani endelevu kwa wanahisa wetu wote na wadau wetu kwa ujumla, tukizingatia vipaumbele vyetu vya huduma bora kwa wateja wetu, urahisi wa kutumia huduma na bidhaa zetu, pamoja na ukuaji endelevu wa biashara yetu. Natazamia safari nyingine ya kusisimua na matokeo mazuri zaidi katika mwaka ujao.



Philip Besiimire
Mkurugenzi Mkuu
17 Julai 2024

Bidhaa na huduma zetu

Tuna wateja zaidi ya milioni 19.6 wanaotumia bidhaa na huduma zetu.

Huduma kwa matumizi ya wateja binafsi na kidigitali



Sauti

- ▷ Simu za kiganjani

Data

- ▷ Modemu za broadband
- ▷ Intaneti kwa simu
- ▷ Intaneti ya majumbani na maofisini

Ujumbe mfupi

- ▷ Ujumbe mfupi wa maneno na programu za mitandao ya kijamii

Huduma za ziada

- ▷ Vyombo vya habari na burudani (habari, video na muziki ya kidigitali na michezo ya bahati nasibu)
- ▷ Elimu na matangazo (Silabu na SmartBango)
- ▷ Huduma binafsi (My Vodacom app, tovuti yetu na Nipige tafu)
- ▷ Afya (Afyacall na Elimika)
- ▷ Huduma za usafiri (Paisha)

Huduma kwa wateja

- ▷ Kituo cha mawasiliano
- ▷ Dawati la huduma kwa wateja
- ▷ Maduka ya Vodacom
- ▷ Huduma binafsi (My Vodacom app, USSD code, M-Pesa app)
- ▷ Huduma za kidigitali (kupitia mitandao ya kijamii, tovuti, Whatsapp na Live Chat app)
- ▷ Viashiria kwa wateja (ujumbe ibukizi)
- ▷ Huduma jumuishi na kaunta maalum kwa wateja wenye mahitaji maalum

M-Pesa



Kuweka na kutoa fedha

- ▷ Kwa mawakala zaidi ya 163 000

Kuhamisha na kupokea fedha kati ya wateja wetu

- ▷ Kutuma pesa ndani ya nchi na kimataifa (IMT)

Huduma binafsi

- ▷ Aplikesheni ya M-Pesa

Mifumo ya malipo ya kielektroniki

- ▷ Kadi za kielektroniki 'M-Pesa VisaCard'
- ▷ Mfumo wa malipo wa 'Lipa kwa Simu'
- ▷ Mteja kwenda kwenye Biashara 'C2B'
- ▷ Biashara kwenda kwa Mteja 'B2C'
- ▷ Biashara kwenda kwa Biashara 'B2B'

Huduma za kifedha

- ▷ Huduma ya mikopo ya Songesha
- ▷ Akiba na mikopo (M-Pawa, M-Godi na Halal Pesa*)
- ▷ Akaunti za akiba za vikundi (M-Koba na Changisha)
- ▷ Mikopo ya muda mrefu ya mawakala
- ▷ Huduma za bima

Matumizi ya wateja wa Biashara



Simu za kiganjani

- ▷ Sauti
- ▷ Vifurushi kwa wateja wadogo wa kibiashara
- ▷ Data
- ▷ Intaneti ya Vitu
- ▷ Ujumbe mfupi wa maneno
- ▷ Huduma binafsi
- ▷ Huduma za ziada

Huduma za data majumbani na maofisini na ukodishaji wa sehemu za rasilimali zetu

- ▷ Huduma za intaneti
- ▷ Uunganishaji wa kampuni na matawi yake
- ▷ Huduma za ukodishaji
- ▷ Huduma za uhifadhi wa rekodi kielektroniki
- ▷ Mkongo maalum kwa ajili ya makampuni
- ▷ Huduma za kidigitali kama M-Kulima na 'Connected schools'

* Akaunti za akiba za Hala Pesa zinafuata miongozo ya Sharia.




Azma yetu

Azma ya Vodacom Tanzania ni 'kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora', na tunapambana kuboresha maisha ya mamilioni ya Watanzania kupitia mpango huu. Mwaka huu, azma yetu imebadilishwa na kulenga nguzo mbili kutoka nguzo tatu za hapo awali. Azma hii iliyoboreshwa inayolenga **'Kuiwezesha jamii'** na **'Kuilinda sayari'**, inatuwezesha kuendelea kutoa huduma bunifu za kidigitali na kifedha ambazo zina uwezo wa kubadili maisha ya watu, huku tukizingatia umuhimu wa uaminifu katika kila tulifanyalo. Zaidi, lengo letu ni utekelezaji wa wajibu wetu kwa jamii kwa kushirikiana na wadau wetu ili kuhakikisha tunatoa michango muhimu katika huduma jumuishi za kidigitali na kifedha.

Kama kampuni ya kidigitali inayoongoza, njia inayofaa zaidi kuongeza kasi ya mabadiliko ya kijamii na kiuchumi na kuchangia vizuri katika malengo ya maendeleo ya taifa na dunia ni kupitia huduma ya mawasiliano inayoaminika, na kuchochea upatikanaji wa huduma jumuishi za kidigitali kimawasiliano na kifedha kupitia M-Pesa.



Kama sehemu ya Kampuni ya Vodafone na Kundi la makampuni ya Vodacom, tumedhamiria kujikita katika maeneo mapana mawili yanayolenga kuchangia katika kufikiwa kwa malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (UN SDGs):



Kupitia shughuli zetu katika maeneo haya, tunatoa mchango mzuri katika malengo yafuatayo ya Maendeleo ya Kimkakati ya Umoja wa Mataifa:





Kuiwezesha jamii

- Thamani iliyotengenezwa
- Thamani iliyopungua
- Thamani endelevu

Kuiwezesha Jamii kwa kujenga 'Jamii iliyunganishwa Kidigitali'

Ili kukuza uchumi wa Tanzania, ni muhimu kupunguza ombwe la kidigitali, hatua itakayotufanya tuufikie uchumi unaoendeshwa kwa uimara wa ujuzi na maendeleo ya viwanda vya kati. Sekta ya mawasiliano ya simu za kiganjani imechangia katika malengo ya maendeleo ya taifa kwa kuwezesha upatikanaji wa huduma jumuishi za kidigitali. Sekta hii bado ina nafasi ya kuchangia zaidi kwa kuongeza upatikanaji wa huduma muhimu, kuongeza uzalishaji katika sekta mbalimbali za kibiashara, na kufungua fursa jumuishi za kiuchumi. Tunaendelea kupunguza ombwe la kidigitali kwa kuongeza upatikanaji wa huduma za kidigitali kupitia uwekezaji wetu katika kupanua miundombinu ya mawasiliano hasa katika maeneo ya vijijini, upatikanaji wa mikopo yetu ya "nipige tafu", kuwezesha upatikanaji wa simu janja za bei nafuu na, upatikanaji wa vifurushi vya gharama nafuu zaidi ili kuwezesha mawasiliano kwa wote. Pia tunatengeneza mifumo maalum ya kidigitali ambayo inasaidia udigitishaji wa biashara, huduma za serikali na sekta muhimu zinazotatua changamoto za kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Huduma za mtandao kwa watu wote

- Mwaka huu, tumewekeza kiasi cha shilingi bilioni 170.1 katika kupanua wigo na kuboresha mtandao wetu. Tumeongeza minara mipya 17 katika maeneo ya vijijini nchini Tanzania na kuendelea kuwezesha upatikanaji bora wa huduma za data kwa kujenga minara mipya 132 ya 5G na minara mipya 451 ya 4G. Pia tumejenga minara mipya 11 katika maeneo maalum kwa kushirikiana na serikali kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote "Universal Communications Service Access Fund (UCSAF)."
- Kufikia mwisho wa mwaka, tulikuwa na jumla ya minara 1 704 maeneo ya vijijini², ikiwemo minara 313¹ iliyojengwa kwa ushirikiano na UCSAF katika miaka kumi na miwili iliyopita ya ushirikiano wetu. Kupitia uwekezaji wetu endelevu unaolenga kupanua wigo wa mtandao na kuongeza uwezo wa mtandao, 72.0%³ ya watazania wamefikwa na mtandao wetu wenye kasi wa data.
- Tumeendelea kuhamasisha huduma jumuishi za kidigitali kupitia vifurushi vyetu vya bei nafuu vinavyotolewa chini ya mwavuli wa huduma ya 'Ya Kwako Tu', inayowezeshwa na mifumo ya CVM na 'machine learning'. Kila mwezi, takribani wateja milioni 9.0 hutumia ofa za Ya Kwako Tu.
- Pia tumeendelea kuwezesha upatikanaji wa huduma ya mkopo wa muda wa maongezi 'Nipige Tafu', ambayo huwezesha wateja kupata huduma za mawasiliano ya simu, kwa kukopa muda wa maongezi au vifurushi na kurejesha pindi atakapoozeka muda wa maongezi. Mwaka huu, wateja karibu milioni 7 wamenufaika kutokana na zaidi ya shilingi bilioni 100 za mikopo ya muda wa maongezi, ambalo ni ongezeko la zaidi ya 16% ikilinganishwa na mwaka jana.
- Tunaendelea na mikakati ya kuwezesha upatikanaji wa vifaa janja kwa gharama nafuu ili kuwawezesha watu wengi zaidi kutumia huduma za data na za kidigitali. Mwaka huu tuliendelea mikakati ya kuongeza watumiaji wa simu janja, hususan kupitia huduma yetu ya mkopo ya simu janja inayowawezesha watumiaji kumiliki simu janja za gharama nafuu, kwa malipo ya awali yanayoanzia shilingi 20 000, na marejesho ya kila siku ya chini ya shilingi elfu moja kwa muda wa miezi 12. Mkakati huu ulichangia ongezeko la 24.3% la watumiaji wa simu janja hadi kufikia milioni 6.6. Tunaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kubaini fursa mpya zitakazochochea uhitaji na kuchangia unafuu wa bei za simu janja.

1. Kumbuka: si minara yote ilijengwa kwa ushirikiano na UCSAF ni minara ya vijijini. Vigezo vikuu vya ufadhili ni kuwezesha huduma katika maeneo yaliyokosa huduma ambayo hayavutii kibiashara; kijiografia hii minara inaweza pia kuwa katika maeneo ya mjini.
2. Fasili ya 'minara ya vijijini' inategemea vigezo vya ndani vya Vodacom na si eneo la kijiografia. Idadi ya 'minara ya vijijini' inaweza pia kubadilika kati ya miaka husika kufuatia mapitio ya ndani na uainishaji mpya.
3. Kipimo kwa Mbps 1.

Kuhamasisha Ujumuishi kifedha

- Tumeendelea kupiga hatua kubwa zaidi mwaka huu katika kuwezesha Ujumuishi kifedha kupitia huduma yetu ya M-Pesa. Zaidi ya wateja milioni 10 wameunganishwa katika huduma rasmi za kifedha kupitia M-Pesa – mtoa huduma za kifedha kwa simu mkubwa zaidi nchini Tanzania. Wateja hao walichakata miamala karibia bilioni 2.0, yenye thamani ya takribani shilingi trilioni 100 kwa mwaka huu.
- Huduma yetu ya M-Pesa imepiga hatua kubwa katika kuchochea huduma jumuishi za kifedha, hususan kwa jamii isiyofikiwa na huduma za kibenki kwa kuwafikishia huduma muhimu za kifedha ambazo kwa kawaida zilikuwa zinapatikana kupitia benki au kampuni za bima tu. Huduma hizo ni pamoja na uhamishaji fedha, malipo kwa wafanyabiashara, akiba binafsi na za vikundi, mikopo ya muda mfupi, na huduma za bima.
 - Huduma yetu ya kuweka akiba ya M-Koba, inayoendeshwa kwa ushirikiano na Tanzania Commercial Bank (TCB) ilianzishwa kwa lengo msingi la kutumika katika vyama vya kijamii vya kuweka akiba na mikopo, kuleta suluhisho la upotevu wa fedha kutokana na utunzaji duni wa kumbukumbu, uhifadhi wa fedha usio salama, wizi na au uaminifu hafifu wa wasimamizi wa vikundi hivyo. Inatia moyo kuona thamani ya miamala katika M-Koba imeongezeka kwa zaidi ya 100% – ambayo ni zaidi ya mara mbili ukilinganisha na mwaka uliopita, ambapo zaidi ya 60% ya thamani ya miamala hiyo ilifanywa na wanawake, ikiakisi uwezeshaji wanawake kwenye jamii yetu unaotokana na huduma ya M-Koba.
 - Kupitia M-Pesa, wateja wetu wa M-Pawa na M-Godi wanapata huduma ya akaunti ya kuweka akiba; zaidi ya shilingi bilioni 400 za akiba ziliwekwa katika huduma hizi mwaka huu.
 - Mwaka huu, zaidi ya wateja milioni 6.0 walinafaika na mikopo yetu ya Songesha, ambayo inapatikana kwa urahisi na haihitaji kujaza fomu au dhamana. Mikopo ya namna mbalimbali yenye thamani ya takribani shilingi trilioni moja iliyotolewa kwa mawakala karibia 100 000, ikiwanufaisha katika uendeshaji wa biashara zao, na kuhakikisha upatikanaji wa huduma kwa wateja wetu.

Azma yetu inaendelea

Udigitishaji wa sekta muhimu

- Mfumo wetu bunifu wa M-Kulima hivi sasa umewaunganisha wakulima wadogo zaidi ya milioni 3.2 waliosajiliwa kwenye mnyororo wa thamani, na kuwawezesha kupata taarifa, huduma na masoko kupitia aplikesheni 'App' na Ujumbe Mfupi 'SMS', na kupokea malipo kwa haraka na salama zaidi kupitia M-Pesa. Kwa kudigitisha jamii ya wakulima, mfumo huu unawawezesha wakulima wadogo na kutoa chanzo muhimu cha takwimu za sekta hiyo kwa serikali ili kuwezesha ukulima wenye tija. Mwaka huu, zaidi ya shilingi bilioni 16 zililipwa kwa wakulima walioisajili kupitia mfumo wa M-Kulima. Tunaendelea kutathmini namna zingine za kudigitisha mnyororo wa thamani wa kilimo ili kunufaisha zaidi jamii za wakulima.
- ✔ Kupitia mfumo wetu wa e-Fahamu (instant schools), tunatoa vifaa mbalimbali vya kidigitali kwa mashule. Shule zilizobainishwa na uhitaji hupatiwa vifaa kwa ajili ya wanafunzi na walimu wake kuweza kuhusuma na kufundisha kwa njia ya mtandao. Jumla ya shule 285 zenye wanafunzi 42 181 waliosajiliwa zinatumia mfumo huu. Katika kuendelea ari yetu hii tulifanya kampeni ya kuongeza ufahamu kuhusu huduma hii iliyowafikia wanafunzi takribani 18 000 na walimu 1 350, huku tukichangia kompyuta za mezani 204, machine za kuchapa 17, vishkwambi 145 na visafirisha data 'routers' 101. Jumla ya uwekezaji wetu katika shughuli za e-Fahamu ulikuwa shilingi milioni 593.

Kudigitisha serikali

- ✔ Huduma zetu za malipo ya kielektroniki kupitia M-Pesa, zikichagizwa na utayari wa serikali kudigitishaji malipo, zimeongeza ufanisi kwa kuwezesha malipo kwa njia ya kielektroniki katika maeneo kama vile huduma ya maji na umeme, elimu na maegesho mijini. Malipo ya serikali kutoka kwa wateja yamerahisishwa kupitia M-Pesa 'super-app' ambayo imeunganishwa moja kwa moja kwenye mfumo wa serikali wa GePG. Mwaka huu, thamani ya miamala ya malipo kwa serikali iliongezeka kwa 22.8% huku wingi wa miamala hiyo ikiongezeka kwa 15.1%.
- Mwaka huu tulipiga hatua ya kuridhisha katika kusukuma udigitishaji wa baadhi ya kazi zetu na serikali na wakala wa udhibiti, na kuleta ufanisi katika kazi. Tutaendelea kufanya kazi na serikali ili kubainisha zaidi fursa za udigitishaji zilizo.

Kuiwezesha jamii kupitia huduma jumuishi kwa wote

Kupitia juhudi zetu mbalimbali za kidigitali zinazoboresha upatikanaji wa mawasiliano, huduma za afya na elimu kwa wote, au kusaidia kampuni chipukizi za kiteknolojia, tunatoa mchango muhimu katika kupunguza umaskini na tofauti za usawa nchini Tanzania.

Ujumuishi katika huduma za mawasiliano

Mbali na kuongezea upatikanaji wa huduma zetu za mawasiliano – kwa kupanua wigo na uwezo wa mtandao wetu, na kuwezesha upatikanaji wa vifaa janja kwa bei nafuu (rejea 'huduma za mtandao kwa watu wote' ukurasa wa 13) – pia kipekee tunahakikisha kunakuwa na upatikanaji na huduma jumuishi kwa wateja wenye mahitaji maalum. Huduma hizi jumuishi ni pamoja na:

- ✔ Kujenga njia zenye kuwezesha viti vya magurudumu kuingia katika maduka zaidi ya 171 nchini (mwaka wa fedha 2023: maduka 80).
- ✔ Kuanzisha huduma ya lugha ya alama kwa ajili ya wateja wenye changamoto ya kusikia, kwa kuwaajiri wataalamu wa lugha ya alama na kutoa mafunzo ya awali kwa wafanyakazi wetu waliopo katika vituo vyetu vya huduma namna ya kuwasiliana kwa lugha hiyo ya alama.

- ✔ Kutoa huduma kwa wateja kupitia WhatsApp ya mwito wa video inayopokelewa na mtaalamu wa lugha ya alama.
- Kuweka kaunta maalum, kwa ajili ya wateja wetu wenye mahitaji maalum.

Jithada hizi zinakusudia kuhakikisha kuwa wateja wetu wanapata fursa sawa za kutumia huduma zetu bila kujali hali ya kimwili. Mwaka huu, kadri ya wateja 7 700 walihudumiwa kupitia huduma zetu jumuishi.

Afya kwa wote

- ✔ Huduma ya M-mama kwa ushirikiano na Vodafone Foundation, USAID na Serikali ya Tanzania, imesaidia kupunguza vifo vya kina mama wawawazito kupitia utoaji wa usafiri wa dharura kwa kina mama wawawazito kwenda kwenye vituo vya afya katika maeneo ya vijijini. Programu hii ilianza mwaka 2013 kama mradi wa majaribio katika mkoa wa Shinyanga na sasa inafanya kazi katika mikoa yote nchini. Mwisho wa huu mwaka wa fedha, jumla ya kesi za dharura 55 000 zilishughulikiwa kupitia programu hii, na kuokoa maisha ya zaidi ya watu karibia 2 000.
- ✔ Kampeni yetu ya kujenga ufahamu wa magonjwa yasio ya kuambukiza kupitia mpango wa "Afya Bora Camp" ilifanyika kwa kufanya ukaguzi wa afya ya jamii bure kwa Watanzania. Kadri ya wananchi 3 500 walihudumiwa kupitia mpango huu, na pale matatizo ya kiafya makubwa yalipogunduliwa, walipewa rufaa kwenda katika hospitali za mikoa. Kampeni hii iliendeshwa kwa ushirikiano na Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Waganga Wakuu wa Mikoa, Chama cha Madaktari Tanzania, Chama cha Wanafunzi wa Udaktari Tanzania, na Chama cha Taasisi Binafsi za Afya Tanzania (APHFTA). Jumla shilingi milioni 129.4 zilitumika katika kampeni hii.

Elimu kwa wote

- Kuimarisha uthabiti wa mtandao wetu wa data nchini kote kunawawezesha wateja wetu kuvifikia vyanzo vizuri vya elimu kupitia intaneti. Kwa kuendelea kupanua wigo wa upatikanaji wa intaneti yenye kasi kubwa kupitia simu za kiganjani na uunganishwaji kwa waya, wateja wetu wanaweza kupata machapisho ya elimu kwa mtandao zikiwemo maktaba za kielektroniki, mihadhara na maudhui mengine ya elimu.
- ✔ Kupitia programu yetu ya 'Code Like A Girl', tunatoa mchango unaolenga kuhamasisha ushiriki wa wasichana katika kazi za sayansi na hesabu (STEM). Tunaunga mkono serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na mashule, kuwahasisha wanawake vijana na wasichana kusoma masomo ya STEM na TEHAMA na kuchochea maendeleo ya huduma za kidigitali kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. Tangu kuzinduliwa kwake, wasichana takribani 2 340 wenye umri wa miaka 14 mpaka 18 wameshiriki katika programu hii, iliyowawezesha kuwa na ujuzi katika misimbo na stadi za maisha, na pia, kuwahasisha kusoma masomo ya TEHAMA na 'STEM'.

Kusaidia biashara chipukizi za kiteknolojia

- ✔ "Digital Accelerator Msimu wa 3" – programu inayoendeshwa kwa ushirikiano na Mass Challenge na Huawei Tanzania, inaazimia kuwasaidia Watanzania wabunifu na wanaoanza biashara kubadili maono yao kuwa biashara yenye thamani ambazo zitatoa nafasi za ajira na kutatua changamoto za kijamii. Kwa misimu mitatu, programu hii imevutia waombaji zaidi ya 750 (210 mwaka huu), huku ikiwasaidia pamoja na kuwapa huduma za ushauri wafanyabiashara chipukizi zaidi ya 35 walioteuliwa (mwaka huu 15), kupitia kambi za mafunzo, maabara za ubunifu (design-thinking labs), maonesho mbalimbali, na vipindi maalum vilivyoandaliwa na washauri wao.

- Thamani iliyotengenezwa
- Thamani iliyopungua
- Thamani endelevu



Kuilinda sayari

Tutaendelea kutunza mazingira ambayo tunafanyia shughuli zetu za kibiashara kwa kuwekeza katika masuala ya tabianchi ikiwemo mitandao na mifumo inayotumia nishati kidogo, kupunguza taka katika mnyororo wetu wa thamani, kuongeza unyumbufu wa tabianchi kwa kupanda miti na kuhakikisha kuwa tunafuata kikamilifu masharti yote ya utunzaji wa mazingira.

Mabadiliko ya tabianchi, na ufanisi katika matumizi ya nishati na maji

Tunaendelea kudhibiti uzalishaji wetu wa hewa ya ukaa na kuongeza ufanisi katika matumizi ya nishati na maji kwa kuboresha vituo vyetu vya data na kuongeza ufanisi katika mtandao wetu. Japokuwa mwaka huu matumizi yetu ya nishati yaliongezeka, hiyo ilitokana na upanuzi wa mtandao wetu. Mwaka huu, tumetekeleza juhudi mbalimbali ambazo zinaleta ufanisi na kuchangia katika lengo la Kampuni yetu mama ya Vodacom, inayolenga kufikia matumizi ya juu kabisa ya usafi ya nishati (Net zero) kwenye makampuni yake yote kufika mwaka 2035.

- Tunashirikiana na watoa huduma yetu kuongeza kasi ya kuunganisha minara katika gridi ya taifa ili kupunguza matumizi ya jenereta zinazotumia dizeli; kwa sasa, 89% ya minara imeunganishwa kwenye gridi ya taifa ambapo, 6% inatumia nishati ya jua.
- Tumeanzisha jitihada mbalimbali za kuongeza ufanisi katika matumizi ya nishati kwenye vituo vyetu vya data na tunatarajia kuunganisha vituo vyetu vyote vya data katika vyanzo vya nishati jadidifu kufika 2026.

- Tumekamilisha mahitaji ya mchakato na kupata hati ya ISO ya Mifumo yetu ya Usimamizi wa Nishati.
- Katika kutekeleza juhudi zetu za kupunguza gharama, tumendelea kuongeza ufanisi wa mtandao na TEHEMA, kwa kutumia na kujenga miundombinu ya mawasiliano hasa minara kwa kushirikiana na watoa huduma wengine, kubuni baadhi ya bidhaa zetu muhimu za TEHAMA, na kudigitisha shughuli zetu mbalimbali za uendeshaji.

Kupunguza uzalishaji taka

- Lengo letu la muda mrefu katika kuwahimiza wateja kubadilika kutoka kutumia vocha za karatasi na kutumia njia za kielektroniki katika kuongeza muda wa maongezi – kama vile M-Pesa, mashine za kutolea pesa (ATM), na Vodafasta – limechangia kupunguza wastani wa tani 214.4 za taka za karatasi mwaka huu, na kusababisha kuepukwa kwa matumizi ya tani zisizopungua elfu moja za karatasi katika kipindi cha miaka minane iliyopita.
- Matumizi ya laini ndogo za simu zilizotengenezwa kwa malighafi inayooza kirahisi, kumepunguza matumizi ya plastiki na taka za plastiki kwa wastani wa tani 30.8 mwaka huu, na kuepusha wastani wa jumla ya tani 210.8 za taka za plastiki katika miaka nane iliyopita.

Viashiria vya uendelevu wa biashara	Kipimo	Machi-24	Machi-23	Machi-22	Machi-21	Machi-20
Idadi ya wafanyakazi	Idadi	607	581	560	569	551
Idadi ya wafanyakazi wanawake	Idadi	231	218	209	203	204
Wanawake kwenye Kamati ya Uongozi (ExCo)	%	38.5	38.5	38.5	36.4	30.8
Wanawake kwenye Menejimenti (ngazi ya Wakuu wa Vitengo na ExCo)	%	46.7	43.8	40.0	41.2	41.2
Wafanyakazi wanawake	%	38.1	37.5	37.3	35.7	37.0
Jumla ya gharama zilizotumika kugharimia wafanyakazi	(Sh bn)	74.7	65.2	63.8	63.8	57.7
Jumla ya matumizi katika mafunzo	(Sh bn)	1.7	0.3	0.2	0.7	1.0
Vifo wakati wa kazi	Idadi	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
Uwajibikaji kwa Bidhaa na Huduma (Customer NPS)	Nafasi	Kwanza	Kwanza	Kwanza	Kwanza	Kwanza
Kiwango cha kuridhika ushirikishwaji wa wafanyakazi	%	94	93	85	86	86
Wateja wote (siku 90)	Idadi ('000)	19 563	16 735	15 368	14 861	15 513
Wateja wa M-Pesa (kwa mwezi)	Idadi ('000)	10 169	8 197	6 833	7 395	6 685
Wateja wa Data (kwa mwezi)	Idadi ('000)	10 065	8 748	7 603	7 695	7 687
Gharama za uwekezaji	(Shi bn)	170.1	156.0	174.0	122.4	154.6
Jumla ya kodi na makato yaliyolipwa serikalini ¹	(Shi bn)	522.6	530.0	516.9	429.7	434.8
Jumla ya mikopo ya muda wa hewani kwa wateja	(Shi bn)	101.7	72.5	68.6	43.3	38.2
Jumla ya thamani iliyopita kwenye M-Pesa	(Shi tn)	97.1	70.4	61.9	69.2	58.9
Wanufaika wa mikopo ya Songesha	Idadi ('000)	6 179	4 444	3 776	3 541	2 001
Minara vijijini (UCSAF)	Idadi	313	302	283	260	217
Minara vijijini (Jumla)	Idadi	1 704 ²	1 687	1 680	1 660	1 570
Wateja wetu walioko vijijini	Idadi	8 987	7 689	7 016	6 719	6 298
% ya wateja wetu walioko vijijini	%	55	54	57	56	53
Matumizi ya karatasi yaliyoepukwa kwa kutumia vocha za kielektroniki	Tani	214	172	134	140	175
Matumizi ya plastiki yaliyoepukwa kwa kutumia laini – SIM-kadi ndogo	Tani	31	29	15	22	30

- Takwimu za mwaka wa fedha 2024 zinajumuisha 'ushuru wa forodha' ambao haukwepo katika miaka iliyotangulia. Bila ushuru huu, thamani ya mchango wetu ingekuwa shilingi bilioni 496.4 – upungufu huu unatokana na kushuka kwa tozo katika huduma za kifedha kwa simu baada ya kuondolewa kwa tozo kwenye huduma za kutuma na kupokea fedha kati ya wateja wetu.
- Taarifa ya masuala ya mazingira, jamii na utawala (ESG) ya makampuni ya Vodacom kwa mwaka wa fedha 2024 imeonesha Vodacom Tanzania ina minara mipya 34 vijijini. Hata hivyo, idadi hii itasasishwa kuwa 17 katika taarifa zijazo.

Taarifa ya Mkurugenzi wa Fedha

Mwaka huu tuliendeleza kasi ya ukuaji wetu iliyopelekea ongezeko la faida baada ya kodi kwa 20%. Licha ya changamoto mbalimbali ikiwemo ongezeko la gharama lililotokana na ongezeko kubwa la viwango vya kubadilishia fedha za kigeni lililotokana na changamoto mbalimbali za kiuchumi na kisiasa duniani, tulifanikiwa kupata matokeo mazuri kifedha yaliyochangiwa na ongezeko la mapato ya huduma pamoja na, juhudi zetu thabiti za kubana matumizi. Nina furaha kuwaleteeni taarifa za ufanisi wetu kifedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024.



Hilda Bujiku

Mkurugenzi wa Fedha

Taarifa za Jumla	2024	2023	Badiliko % la mwaka hadi mwaka
Mapato ya huduma (Sh m) ambapo	1 258 335	1 053 762	19.4
Mapato ya huduma za simu kwa sauti (Sh m)	285 769	278 246	2.7
Mapato ya M-Pesa (Sh m)	456 285	357 136	27.8
Mapato ya data za simu (Sh m)	347 303	273 702	26.9
Mapato ya huduma za kidigitali na huduma za ziada (Sh m)	38 723	35 797	8.2
Mapato ya simu zinazolingia (Sh m)	48 380	46 340	4.4
Mapato ya data za majumbani na maofisini (Sh m)	30 745	19 509	57.6
Jumla ya mapato (Sh m)	1 278 217	1 073 018	19.1
Faida ya mwaka (Sh m)	53 427	44 556	19.9
Gharama za uwekezaji (Sh m) ¹	170 134	155 981	9.1
Asilimia ya gharama za uwekezaji (%)	13.3	14.5	(1.2)
Nafasi yetu kwa idadi ya wateja katika soko ² (%)	Kwanza	Kwanza	
Idadi ya wateja hai/amilifu ³ (maelfu)	19 563	16 735	16.9
Idadi ya wateja hai/amilifu wa M-Pesa kwa siku 30 ⁴ (maelfu)	10 169	8 197	24.1
Idadi ya wateja hai/amilifu wa data ⁵ (maelfu)	10 065	8 748	15.1
Dakika zilizotumika kwa mwezi ⁶	285	275	3.6
Wastani wa kipato kutoka kwa mteja – ARPU ⁷ (shilingi kwa mwezi)	5 523	5 328	3.7
Idadi ya wafanyakazi	607	581	4.5

Maelezo:

- Matumizi ya mtaji kama asilimia ya mapato.
- Kwa mujibu wa takwimu za mawasiliano za robo mwaka za Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania za Machi 31, 2024.
- Wateja hai wanatokana na jumla ya idadi ya watumiaji wa simu waliofanya miamala inayotowza katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita. Hii ni pamoja na wateja wanaolipa ada ya kila mwezi ambayo inawapa haki ya kutumia huduma husika hata kama kiuhalisia hawaitumii huduma hiyo na wale wateja ambao wanawasiliana nje ya mtandao.
- Wateja hai wa M-Pesa wanatokana na idadi ya watumiaji wa kipekee waliotumia M-Pesa na kufanya miamala inayotowza katika kipindi cha mwezi.
- Wateja hai wa data wanatokana na idadi ya watumiaji wa kipekee wanaozalisha data inayotolewa ankara katika mwezi. Pia ni pamoja na watumiaji katika mpango wa pamoja wa watumiaji au ambao wanatumia APN ya shirika na watumiaji ambao wametengewa bando ya data inayozalisha mapato katika mwezi. Mtumiaji anatambulika kuwa hai kama analipa ada ya mwezi kulingana na mkataba kwa huduma husika au ametumia huduma hiyo katika mwezi huo.
- Dakika za matumizi kwa mwezi hukokotolewa kwa kugawanya jumla ya dakika zilizotumika kwa mwezi kwa wastani wa watumiaji wa dakika hizo katika kipindi hicho.
- ARPU inakotolewa kwa kugawa wastani wa mapato ya huduma kwa mwezi kwa wastani wateja hai katika hicho kipindi.
- Net promoter score ('NPS') ni kipimo kuanzia – 100 hadi 100 ambacho kinaonesha utayari wa wateja kupendekeza bidhaa au huduma za mtoa huduma kwa watu wengine. Inatumika kama kigezo cha kupima hali ya kuridhika kwa wateja na bidhaa au huduma za mtoa huduma imani ya wateja kwa chapa hiyo. Kwa kila mtoa huduma, majibu yanakusanywa kutoka kwa wateja ambao wanatumia bidhaa au huduma zake kama njia kuu au mbadala ya mawasiliano ya simu ('mtumiaji mkuu' au 'mtumiaji mbadala'). Majibu kutoka kwa watumiaji wakuu na watumiaji mbadala yanalinganishwa/pimwa kwa uwiano asilia wa watumiaji wakuu na watumiaji mbadala wa mtoa huduma huyo ili kukokotoa NPS.

Mapato

Mapato ya Huduma yaliongezeka kwa 19.4% hadi shilingi bilioni 1 258.3, yakichagizwa na kasi yetu kibiashara iliyopelekea ongezeko kubwa la wateja na wastani wa mapato kwa kila mteja (ARPU). Juhudi zetu kibiashara zililolenga kuongeza wateja wapya na kulinda idadi ya wateja wetu, na vilevile kuongeza matumizi yao ya bidhaa zetu, lilipelekea ongezeko la wateja kwa 16.9% na ongezeko la wastani wa mapato kwa kila mteja wetu kwa 3.7%.

Mapato ya huduma za simu kwa sauti¹ yaliongezeka kwa 2.7% hadi shilingi bilioni 285.8 yakichagizwa zaidi na juhudi zetu kibiashara za kuongeza wateja, huku mapato ya sauti kutoka kwa kila mteja (ARPU) yakipungua kwa 9.4%. Kupungua kwa mapato ya sauti kutoka kwa kila mteja kulitokana na kushuka kwa wastani wa bei kwa dakika kwa 15%, ikiikisi muendeleo wa shinikizo la bei ya miito ya sauti sokoni, ambayo kwa kiasi yalifidiwa na ongezeko la 6.5% katika dakika zilizotumika kwa kila mteja.

Mapato ya M-Pesa yaliongezeka kwa 27.8%, hadi kufikia shilingi bilioni 456.3, huku mchango wake katika mapato ya huduma ukiongezeka kwa alama za asilimia 2.4 hadi kufikia 36.3%. Ongezeko hili lilichochea na ukuaji wa wateja wa M-Pesa kwa 24.1% pamoja na, ongezeko la mapato ya M-Pesa kutoka kwa kila mteja wa M-Pesa kwa 3.0%. Haya yote yanaikisi ongezeko la matumizi ya huduma zetu mpya ndani ya M-Pesa. Mkazo mkubwa tuliouweka katika huduma zetu mpya ndani ya M-Pesa ambazo ni pamoja na mikopo, bima, uwekaji akiba na malipo kwa wafanyabiashara uliendelea kusaidia kukua kwa wigo wa mapato ya M-Pesa. Mwaka huu, huduma hizi mpya ndani ya M-Pesa zimechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la mapato ya M-Pesa.

Mapato ya data za simu yalichangia kwa kiasi kikubwa mapato ya mwaka huu, yakiongezeka kwa 26.9% hadi shilingi bilioni 347.3, huku mchango wake katika mapato ya huduma ukiwa 27.6% kutoka 26.0% mwaka uliopita. Ufanisi wa mapato ya data ulitokana na mafanikio ya utekelezaji kibiashara, kuikiwa na ongezeko la wateja la 15.1% hadi milioni 10.1 na pato la data kutoka kwa kila mteja likikua kwa 10.3%. Ongezeko la mapato ya data kutoka kwa kila mteja lilichochea zaidi na ongezeko la matumizi ya data kwa kila mteja, likiwezesha na uwekezaji wetu katika mtandao na ongezeko la watumiaji wa simu janja.

Mapato ya huduma za kidigitali na huduma nyingine za ziada yanayojumuisha mkopo wa muda wa hewani – nipige tafu na huduma za ziada (VAS) yaliongezeka kwa 8.2% hadi shilingi bilioni 38.7. Ongezeko hili lilichangiwa na wigo mpana wa bidhaa zetu kutoka huduma zetu za kidigitali na huduma zingine za ziada, likiwezesha na utekelezaji wetu kibiashara.

Mapato ya simu zinazolingia yaliongezeka kwa 4.4% hadi shilingi bilioni 48.4 yakichochea na ongezeko la 14.6% la idadi ya dakika za simu zinazolingia kutoka mitandao mingine. Ongezeko la mapato kiasi fulani lilisawazishwa na kupungua kwa 5.4% kwa gharama zinazotowza kwa dakika, kwa simu zinazolingia kutoka mitandao mingine kutoka shilingi 1.86 hadi shilingi 1.76 kwa dakika mnamo Januari 2024.

Mapato ya data za majumbani na maofisini yalipata ongezeko thabiti la 57.6% hadi kufikia shilingi bilioni 30.7. Ufanisi huu unaikisi uwekezaji wetu katika miundombinu iliyofungwa pasi waya, ambapo wateja waliounganishwa na mtandao wetu wa data majumbani na maofisini waliongezeka kwa zaidi ya 35%.

Faida ya mwaka

Tulipata faida baada ya kodi ya shilingi bilioni 53.4, ikiwa ni ongezeko la 19.9%. Ukuaji wa faida unaikisi ongezeko thabiti la mapato yetu ya huduma na juhudi zetu za kubana matumizi, ambapo zaidi ya shilingi bilioni 70 ziliokolewa. Akiba iliyopatikana kwa kubana matumizi, ilisaidia kwa kiasi fulani kupunguza shinikizo la ongezeko la gharama lililotokana na ongezeko la bei za nishati, marekebisho ya mfumuko wa bei kwenye mikataba ya huduma iliyopo, na athari zilizotokana na ongezeko kubwa la viwango vya kubadilisha fedha za kigeni.

Gharama za uwekezaji²

Mwaka huu, tuliwekeza shilingi bilioni 170.1 katika miundombinu yetu, sawa na 13.3% ya mapato yetu. Matumizi haya yalielekezwa katika kuongeza wigo wa mtandao wetu wa data, kuongeza uwezo na kuboresha miundombinu yetu ya TEHAMA. Tulijenga minara mipya 451 ya 4G na kuongeza kilomita 250 za mkongo. Pia, tuliwekeza katika kuboresha mfumo wa TEHAMA ili kusaidia maendeleo ya bidhaa bunifu, pamoja na bidhaa za kidigitali na kifedha katika siku zijazo. Tuna furaha kuwa uwekezaji wetu endelevu ulisaidia ukuaji wa biashara na mabadiliko ya matumizi kwa watumiaji wetu wa data kutoka 3G na kwenda 4G, jambo linatosukuma mahitaji zaidi ya data kupitia huduma bora kwa wateja. Mwaka huu, mtandao wetu wa 4G ulisafirisha zaidi ya 75% ya jumla ya data ikilinganishwa na matumizi yaliyokuwa chini ya 66% mwaka uliopita.



1. Kwa kuzingatia mabadiliko na ukuaji wa programu yetu ya kuvuna Tuzo pointi katika miaka ya hivi karibuni, imekuwa sahihi zaidi kuonyesha mapato yake ndani ya mapato mengine badala ya mapato ya simu kwa sauti. Hivyo, mapato yake ya shilingi bilioni 5.9 bilioni na shilingi bilioni 5.3 kwa mwaka wa fedha 2024 na 2023, yamejumuishwa ndani ya mapato mengine. Hakuna athari yeyote kwenye mapato ya huduma kutokana na marekebisho haya.
2. Gharama mbali na gharama za kununua na kuungana na Kampuni nyingine, pamoja na mabadiliko katika wadeni wetu katika uwekezaji wa mali na mitambo.

Taarifa ya Mkurugenzi wa Fedha inaendelea

Muhtasari wa taarifa zote za kifedha

Muhtasari wa faida au hasara na mapato mengine

Sh m	Zimekaguliwa 2024	Zimekaguliwa 2023
Mapato	1 278 217	1 073 018
Jumla ya gharama	(882 564)	(740 261)
Gharama za moja kwa moja	(418 035)	(349 470)
Gharama za wafanyakazi	(74 666)	(65 230)
Gharama za kujitangaza	(30 358)	(27 255)
Gharama za kukodisha na uendeshaji wa minara	(141 017)	(121 532)
Gharama zingine za uendeshaji	(218 488)	(176 774)
Uchakavu	(260 317)	(248 306)
Gharama za madeni chechefu	(1 060)	(2 974)
Faida za uendeshaji	134 276	81 477
Mapato ya kifedha	25 764	24 463
Gharama za kifedha	(73 107)	(76 650)
Hasara kutokana na mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha za kigeni	(8 949)	(2 940)
Faida kabla ya kodi	77 984	26 350
(Gharama)/unafuu wa kodi ya mapato	(24 557)	18 205
Faida ya mwaka	53 427	44 556
Mapato mengine	-	-
Jumla ya faida halisi kwa mwaka wa mapato, baada ya kutoa kodi¹	53 427	44 556
Mapato ya msingi na mchanganyiko kwa kila hisa (Sh)	23.83	19.89

Tumezalisha mapato ya shilingi trilioni 1.3 ikiwa ni ongezeko la 19.1%, kwa kiasi kikubwa likisababishwa na ukuaji wa mapato ya huduma kwa 19.4%. Juhudi zetu za kibiashara zilizolenga kuongeza wateja na matumizi yao ya huduma zetu zilipelekea ongezeko la wateja kwa 16.9% na ukuaji wa wastani wa mapato kutoka kwa kila mteja hai kwa 3.7%, ambayo kwa pamoja vilichochea ukuaji wa mapato ya huduma. Jambo la kutia moyo ni kwamba, mapato yanayotokana na huduma mpya zinazopatikana kwenye M-Pesa, huduma za kidigitali, pamoja na huduma za data majumbani na maofisini ziliendelea kukua, na kuchangia 25.1% ya mapato yetu ya huduma, sawa na ukuaji wa alama za asilimia 5.6 kutoka mwaka uliopita, muendelezo wa juhudi zetu katika kutanua wigo wa mapato yetu.

Mwaka huu gharama ziliongezeka kwa 19.2% hadi shilingi bilioni 882.6 zikiakisi ukuaji wa biashara, na kwa kiasi, zikipunguzwa na zaidi ya shilingi bilioni 70 zilizoakolewa kutokana na jitihada zetu za kudhibiti matumizi. Vichochezi vikuu vya ukuaji wa gharama ni pamoja na hasara tulizopata kwenye kubadilisha fedha za kigeni kufuatia kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni, kupanda kwa gharama za nishati na kama ilivyotarajiwa, ongezeko la gharama uliosababishwa na ushindani katika soko. Pia, kulikuwa na ongezeko la shilingi bilioni 2.3 kutokana na mabadiliko ya kiwango cha ada zinazolipwa kwa serikali ili kuchangia katika mfuko wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa wote. Vichochezi vingine vya ongezeko la gharama vilitokana na marekebisho ya mfumuko wa bei katika mikataba ya huduma na ujira, ongezeko katika mikataba ya huduma, pamoja na gharama kubwa za nishati katika vituo vyetu vya kuhifadhi rekodi kielektroniki kutokana na ongezeko la matumizi ya mafuta kulikosababishwa na mgao wa umeme na pia, ongezeko la bei ya mafuta.

Ongezeko la gharama za uchakavu kwa 4.8% hadi shilingi bilioni 260.3 linaakisi uwekezaji wa ziada uliofanywa katika mtandao, mifumo ya TEHAMA na masafa mapya tuliyonunua.

Gharama za madeni chechefu zinahusisha kiasi kilichotengwa kwa ajili ya hasara tarajiwa za madeni chechefu. Upungufu katika mwaka huu umetokana na ukusanyaji wa madeni chechefu yaliyokuwa yamehesabika kuwa hasara hapo awali.

Mapato ya kifedha yaliongezeka kwa 5.3% ikiwa ni riba kutokana na amana ya wateja wa M-Pesa iliyoko benki ikisaidia kufidia mapato madogo ya riba kutokana uwekezaji mdogo katika amana, uliochangiwa na fedha nyingi zilizotumika katika manunuzi ya masafa na ulipaji wa gawio kwa mwaka wa fedha 2023. Mapato ya kifedha katika salio la kibenki la M-Pesa yalioanishwa na gharama za kifedha katika salio hilo pia.

Mapato ya kifedha yalipungua kwa 4.6% kufuatia kupungua kwa riba ya madeni ya pango kutokana na ulipaji wa madeni hayo.

Gharama za kodi kiasi cha shilingi bilioni 24.6 (mwaka wa fedha 2023: unafuu wa kodi wa kiasi cha shilingi bilioni 18.2) zinaakisi ongezeko la kodi kutokana na kuongezeka kwa faida ya kampuni yetu tanzu ya M-Pesa. Unafuu wa kodi kwenye mwaka uliopita ulitokana na ahirisho la kodi ya shilingi bilioni 50.9 unaohusiana na hasara ya kikodi ya biashara ya GSM ambayo inatarajiwa kupata ongezeko la faida katika muda wa kati, ikifidia gharama za kodi zinazohusiana na kampuni yetu tanzu ya M-Pesa.

Imeongezeka kutokana na hasara tulizopata kwenye kubadilisha fedha za kigeni kufuatia kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni.

1. Ambapo shilingi milioni 40 ni stahiki ya wenyehisa chache.

Muhtasari wa taarifa za pamoja za hali ya kifedha

Sh m	Zimekaguliwa 2024	Zimekaguliwa 2023
Mali		
Mali za kudumu	1 268 668	1 314 691
Thamani isiyoshikika ya uwekezaji	1 639	1 639
Mali na mitambo	595 659	593 185
Mali zisizoshikika	280 069	210 233
Haki ya matumizi ya mali kabla ya kutumia	270 992	371 991
Madeni ya 'Haki ya matumizi' kabla ya kutumia	29 159	40 339
Madeni ya kibiashara na madeni mengine	12 800	11 853
Kodi ya mapato inayotarajiwa kurejeshwa	36 120	33 098
Kodi iliyoahirishwa	42 230	52 353
Mali za muda mfupi	1 107 067	897 149
Malipo ya 'Haki ya matumizi' kabla ya kutumia	12 756	16 916
Mali ghalani	3 409	3 075
"Madeni ya kibiashara na madeni mengine ya kulipwa"	114 380	115 771
Kodi ya mapato inayotarajiwa kurejeshwa	24 532	15 439
Rasilimali za kifedha – M-Pesa	730 293	509 358
Fedha taslimu na mbadala wa fedha	221 697	236 590
Jumla ya mali	2 375 735	2 211 840
Mtaji na Madeni		
Akiba ya mtaji		
Mtaji wa hisa	112 000	112 000
Malipo ziada kwenye hisa	442 435	442 435
Mchango wa mtaji	27 698	27 698
Ziada ya faida iliyotunzwa	270 660	239 590
Mtaji stahiki kwa wamiliki wa kampuni	852 793	821 723
Stahiki ya wenyehisa chache	41	–
Jumla ya mtaji	852 834	821 723
Madeni ya muda mrefu	297 883	400 225
Madeni ya pango	281 831	394 137
Madeni mengine ya kifedha	9 292	–
Tahadhari ya madeni	6 760	6 068
Ruzuku za serikali	–	20
Madeni ya muda mfupi	1 225 018	989 892
Madeni ya pango	110 931	99 203
Madeni mengine ya kifedha	2 930	–
Deni la malipo ya leseni	–	72 168
Ruzuku za serikali	735	513
Madeni ya biashara yanayohusu M-Pesa	730 293	509 358
Madeni ya biashara na mengine ya kulipa	374 540	301 026
Malipo ya gawio	269	–
Tahadhari ya madeni	5 320	7 624
Jumla ya madeni	1 522 901	1 390 117

Ongezeko limetokana na uwekezaji uliofanyika mwaka huu, ukipunguzwa kwa kiasi na gharama za uchakavu.

Ongezeko limechangiwa kwa kiasi kikubwa na masafa mapya tuliyoypata kupitia ununuzi wa Smile Communication Tanzania Limited.

Upungufu umechagizwa zaidi na malipo ya mikataba ya ukodishaji wa sehemu ya minara na pango iliyoisha muda wake.

Upungufu umetokana hasa na matumizi kwa kiasi ya gharama zililolipwa awali za huduma ya miundombinu ya mkongo iliyokodishwa.

Upungufu umetokana hasa na matumizi kwa kiasi ya gharama zililolipwa awali za huduma ya miundombinu ya mkongo iliyokodishwa.

Ongezeko limetokana na kukua kwa mfumo wa huduma zetu za fedha kwa simu likichagizwa na jitihada zetu endelevu za kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma hizo.

Upungufu umechagizwa zaidi na malipo yaliyosalia ya 50% ya masafa tuliyoypata katika mnada uliofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania katika mwaka wa fedha uliopita, ukifidiwa kwa kiasi na ongezeko la fedha taslimu kutokana na uendeshaji wa biashara.

Ongezeko limechangiwa na faida ya mwaka, ambalo kwa kiasi lilipunguzwa na gawio la shilingi bilioni 22.3 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2023 ambalo lililipwa Oktoba 2023.

Upungufu ulichangiwa zaidi na malipo ya mikataba ya ukodishaji iliyoisha muda pamoja na uhamisho wa deni la muda mrefu kuwa deni la mikataba ya ukodishaji ya muda mfupi.

Ongezeko hili limetokana hasa na tofauti ya muda wakati wa malipo na kuhamishwa kwa deni kutoka mikataba ya ukodishaji ya muda mrefu.

Malipo haya kwa serikali yanahusisha malimbikizo ya nyuma ya gharama za miundombinu ya mkongo yatakayolipwa ndani ya muda wa miaka mitano na hivyo kuhamishwa kutoka malimbikizo ya gharama na kuwa madeni mengine ya kifedha.

Haya ni malipo yaliyosalia ya 50% ya masafa tuliyoypata katika mnada uliofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania katika mwaka wa fedha uliopita, ambayo yalilipwa Aprili 2023 kulingana na mkataba wa manunuzi.

Ongezeko limetokana na kukua kwa mfumo wa huduma zetu za fedha kwa simu likichagizwa na jitihada zetu endelevu za kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma hizo.

Ongezeko hili lililusiana zaidi na kiasi kinacholipwa kwa Smile Telecoms Holdings Limited na Smile Telecoms IP Limited kufuatia ununuzi wa Smile Communication Tanzania Limited.

Taarifa ya Mkurugenzi wa Fedha inaendelea Muhtasari wa taarifa zote za kifedha unaendelea

Muhtasari wa taarifa za pamoja za mzunguko wa fedha

Sh m	2024	2023	
Mzunguko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji	643 087	391 390	Ongezeko lilichangiwa na matokeo chanya kibiashara pamoja na ongezeko la mapato kutoka kwa wateja wetu, ambalo kwa kiasi lilipunguzwa na malipo kwa wadani wetu.
Malipo ya kodi ya mapato	(26 549)	(17 050)	
Riba kwenye malipo ya kodi	-	(277)	
Mzunguko ghafi wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji			
Mzunguko ghafi wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji	616 538	374 063	Upungufu umetokana kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya kiuhasibu ambapo malipo ya awamu ya kwanza ya ununuzi wa masafa, yaliripotiwa chini ya 'mzunguko wa fedha zilizotumika katika shughuli za uwekezaji' katika mwaka uliopita, na malipo ya awamu ya mwisho mwaka huu yameripotiwa chini ya 'mzunguko wa fedha kutokana na shughuli za ugharimiaji' - kadri ya matakwa ya makubaliano ya malipo. Ukiondoa athari za mabadiliko haya, ongezeko la gharama za uwekezaji lingekua kwa 11.9% ikilinganishwa na mwaka uliopita, likiakisi uwekezaji endelevu unaolenga kuchochea ukuaji wa biashara.
Mzunguko wa fedha zilizotumika katika shughuli za uwekezaji			
Nyongeza katika mali na mitambo, na mali zisizoshikika	(179 916)	(228 263)	
Mali zilionunuliwa	(12 501)	-	Hii ni ada iliyolipwa kama gharama ya masafa tuliyoypata kupitia ununuzi wa Smile Communication Tanzania Limited.
Mapato kutokana na mauzo ya mali na mitambo	419	500	
Ruzuku za serikali zilizopokelewa	14 456	4 143	Hii ni ruzuku ya 50% kutoka serikalini iliyopokelewa kuhusiana na miradi ya serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, kwa ajili ya kujenga minara mipya kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa na mawasiliano, pamoja na kuboresha minara ya teknolojia ya 2G na 3G ili ifikie teknolojia ya 4G.
Mapato ya fedha yaliyopokelewa	4 409	7 792	
Kuongezeka kwa fedha zilizowekwa kwenye akiba za matumizi maalum	(220 935)	(73 272)	
Riba kutoka amana za M-Pesa	21 355	16 671	
Mzunguko halisi wa fedha katika shughuli za uwekezaji	(372 713)	(272 429)	Ongezeko limetokana na kukua kwa mfumo wa huduma zetu za fedha kwa simu likichagizwa na jitihada zetu endelevu za kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma hizo.
Mzunguko wa fedha kutokana na shughuli za ugharimiaji			
Gawio tulilolipa	(22 265)	(203)	Hii inahusiana na gawio la faida lililotangazwa na kulipwa kwa wanahisa. Takwimu za mwaka uliopita zinazohusiana na malipo ya gawio yaliyosalia ambayo baadaye yalilipwa kwa wanahisa stahiki.
Mkopo wa muda mfupi	47 266	-	
Rejesho la mkopo wa muda mfupi – mtaji	(47 266)	-	Hii inahusiana na mkopo tuliopewa na kuulipa ndani ya mwaka wa fedha huu pamoja na riba ili kusaidia ununuzi wa Kampuni ya Smile Communication Tanzania Limited.
Rejesho la riba ya mkopo wa muda mfupi	(1 312)	-	
Rejesho la madeni mengineyo – mtaji	(771)	-	
Rejesho la riba la madeni mengineyo	(280)	(39)	
Riba ya madeni ya pango iliyolipwa*	(47 774)	(57 098)	Gharama hii inahusiana na hatua za kukabiliana na athari za kupanda kwa ada ya kubadilisha fedha za kigeni dhidi ya shilingi katika soko.
Gharama ya kinga ya kukabiliana na athari za kushuka kwa thamani ya shilingi	(5 767)	-	
Rejesho la deni la leseni ya masafa yaliyonunuliwa	(75 465)	-	Haya ni malipo yaliyosalia ya 50% ya leseni ya masafa tuliyoypata katika mnada uliofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania katika mwaka wa fedha uliopita. Malipo ya awamu ya kwanza yaliyofanyika katika mwaka wa fedha uliopita yaliripotiwa chini ya 'mzunguko wa fedha zilizotumika katika shughuli za uwekezaji'. Mabadiliko katika kuripoti malipo ya awamu ya pili chini ya 'mzunguko wa fedha kutokana na shughuli za ugharimiaji' mwaka huu, ni kwa mujibu wa matakwa ya makubaliano ya malipo.
Rejesho la riba ya deni ya leseni ya masafa yaliyonunuliwa	(1 925)	-	
Malipo ya madeni ya pango – mtaji*	(87 070)	(48 140)	
Riba iliyolipwa kwa wateja wa M-Pesa	(19 596)	(15 556)	
Mzunguko halisi wa fedha zilizotumiwa katika shughuli za ugharimiaji	(262 225)	(121 036)	Ongezeko linaakisi kukua kwa amana za wateja wa M-Pesa.
Punguzo ghafi katika fedha na fedha mbadala	(18 400)	(19 402)	
Fedha taslimu na fedha mbadala mwanzoni mwa mwaka wa fedha	236 590	256 961	
Athari za mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha katika fedha taslimu na fedha mbadala zilizo katika fedha za kigeni	3 507	(969)	
Fedha taslimu na fedha mbadala kufika tarehe 31 Machi	221 697	236 590	

* Ongezeko la malipo ya mikataba ya ukodishaji minara na pango (riba na mtaji) kwa kiasi kikubwa linatokana na tofauti ya muda wakati wa malipo ya mikataba hiyo.



Viongozi wetu

Tuna Bodi yenye wakurugenzi 12, wengi wao ni wakurugenzi wasio watendaji. Mwenyekiti wetu ni mkurugenzi huru.

Muundo wa Bodi

Wakurugenzi watendaji



Mwenyekiti

Thomas B Mihayo (77) N
Aliteuliwa mwezi Novemba 2020


- Utaalamu wa Sheria
- Msuluhishi
- Mahusiano na serikali



Mkurugenzi Mtendaji

Philip Besimire (49)
Aliteuliwa mwezi Oktoba 2022

- Uongozi kimataifa na uzoefu katika uendeshaji wa biashara
- Utekelezaji wa mabadiliko ya kimkakati ya biashara
- Utekelezaji wa mikakati ya kibiashara akiwa na rekodi ya kipekee katika ukuzaji wa biashara



Mkurugenzi wa Fedha

Hilda Bujiku (45)
Aliteuliwa mwezi Januari 2022

- Ujuzi mkubwa wa masuala ya fedha
- Uzoefu mpana katika masoko yanayoibukia

Wakurugenzi huru



Kanini Mutooni (48) A R N
Aliteuliwa mwezi September 2022

- Utaalamu wa fedha na mitaji ya ubia
- Mjumbe wa bodi mwenye uzoefu wa uongozi kimataifa



Margaret Ikongo (66) A
Aliteuliwa mwezi Novemba 2017

- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika
- Uzoefu katika utekelezaji wa shughuli za uendeshaji na mikakati
- Utaalamu wa fedha



Thembeka Semane (48) A
Aliteuliwa mwezi Novemba 2017

- Utaalamu wa fedha
- Mahusiano na serikali
- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika


■ Mwenyekiti

□ Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

□ Kamati ya Ujira

□ Kamati ya Uteuzi

Jinsia



Muundo wa Bodi



Mahudhurio ya vikao vya bodi



Wakurugenzi wasio watendaji



Diego Gutierrez (48)

R

Aliteuliwa mwezi Machi 2018

- Mpanga mikakati ya kibiashara
- Maarifa mapana kuhusu teknolojia ya simu na uzoefu wa masoko yanayoibukia
- Utaalamu wa uongozi wa kimkakati



Sudhersen Ramasamy (38)

Aliteuliwa mwezi January 2022

- Utaalamu wa fedha na mipango
- Uzoefu wa miaka 12 katika kundi la makampuni ya Vodacom



Matimba Mbungela (52)

R N

Aliteuliwa mwezi Agosti 2017

- Maarifa na uzoefu mpana wa usimamizi wa vipaji
- Utaalamu katika taratibu bora za kusimamia rasilimali watu
- Uzoefu katika uendeshaji wa shughuli za kimataifa



Nkateko Nyoka (61)

Aliteuliwa mwezi Aprili 2020

- Uzoefu katika sheria na sera za umma.
- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika
- Uongozi na mahusiano na wadau

Katibu wa Kampuni



Sitholizwe Mdlalose (44)

Aliteuliwa mwezi Julai 2022

- Kiongozi mwerevu wa biashara
- Miaka 19 ya uzoefu katika usimamizi na ushauri wa fedha, ambapo 13 katika sekta ya mawasiliano ya simu katika masoko yaliyokua na yanayoibukia
- Utekelezaji madhubuti wa bidhaa za kibunifu na huduma mpya



Raisibe Morathi (55)

Aliteuliwa mwezi Novemba 2020

- Uzoefu wa masuala ya fedha kimataifa
- Utaalamu wa uongozi kimkakati
- Utaalamu katika kung'amua fursa za kuunganisha au kununua biashara



Caroline Mduma (46)


Aliteuliwa mwezi Aprili 2017

- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika

Miaka

35 – 39	1
40 – 49	6
50 – 59	2
60 na zaidi	3

Muda waliohudumu kwenye nafasi hizi



Kamati ya Utendaji



Philip Besimire (49)

Alijiunga Vodacom mwaka 2022

Mkurugenzi Mtendaji



Hilda Bujiku (45)

Alijiunga Vodacom mwaka 2012

Mkurugenzi wa Fedha



Linda Riwa (36)

Alijiunga Vodacom mwaka 2017

**Mkurugenzi wa Biashara –
Wateja Binafsi**



Epimack Mbeteni (45)

Alijiunga Vodacom mwaka 2014

Mkurugenzi wa Biashara – M-Pesa



Arjun Dhillon (44)

Alijiunga Vodacom mwaka 2017

**Mkurugenzi wa Biashara –
Wateja wa Kibiashara**



Andrew Lupembe (50)

Alijiunga Vodacom mwaka 2007

Mkurugenzi Masuala ya Mtandao



Olaf Mumburi (48)

Alijiunga Vodacom mwaka 2008

Mkurugenzi wa Sheria na Udhibiti



Zuweina Farah (37)

Alijiunga Vodacom mwaka 2023

**Mkurugenzi wa Masuala ya
Mahusiano na Taasisi ya Vodacom**



Harriet Atweza Lwakatare (46)

Alijiunga Vodacom mwaka 2012

Mkurugenzi Huduma kwa Wateja



Vivienne Penessis (48)

Alijiunga Vodacom mwaka 2018

Mkurugenzi Rasilimali Watu



Nguvu Kamando (49)

Alijiunga Vodacom mwaka 2002

**Mkurugenzi wa Huduma za
Kidigitali**



Tax Agapinus (59)

Alijiunga Vodacom mwaka 2020

**Mkurugenzi Dharura na
Utekelezaji**




Athumani Mlinga (56)

Alijiunga Vodacom mwaka 2003

Mkurugenzi TEHAMA

Muundo wa Kamati ya Utendaji


Jinsia




Miaka



Utaifa



Muda waliohudumu kwenye nafasi hizi



Taarifa ya uongozi wa kampuni

Taarifa ya utekelezaji

Vodacom Tanzania Public Limited Company ('Vodacom Tanzania') inajizatiti kutoa huduma zenye ubora wa hali ya juu kwa uaminifu, maadili na utaalumu katika biashara.

Kanuni za uongozi wa kampuni zinajumuisha nidhamu, uhuru wa maamuzi, uwajibikaji, usawa, uwajibikaji kwa jamii, uwazi na uwajibikaji wa wakurugenzi kwa wadau. Kanuni hizi zinazingatiwa katika taratibu za udhibiti wa ndani na sera za Vodacom Tanzania zinazoongoza utendaji wa kampuni na zinawiana na miongozo ya Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana kuhusu taratibu za usimamizi wa shirika unaofanywa na kampuni za umma zilizoordheshwa nchini Tanzania.

Maadili ya viongozi

Bodi inakubali uwajibikaji wa pamoja katika kueleza namna ambavyo maadili na tabia za kimaadili zinapaswa kutekelezwa katika kampuni. Hii ni pamoja na kupanga taratibu za utendaji wa wajumbe wa bodi ili kuhakikisha kuwa wanatenda kwa uadilifu, uzoefu, uwajibikaji, haki na uwazi. Sifa hizi ni kipimo cha maadili kinachozingatiwa katika tamaduni za uendeshaji wa kampuni.

Uongozi na Kamati za Bodi

Bodi

Vodacom Tanzania ina bodi yenye wakurugenzi 12, ambapo kati yao wanne (pamoja na Mwenyekiti) ni wakurugenzi huru wasio watendaji, sita kati yao si watendaji (lakini si huru kwa kuwa wanawakilisha wadau wakuu), na wawili ni wakurugenzi watendaji.

Bodi imeridhika kuwa uwiano wa wataalamu wenye maarifa, ujuzi na uzoefu wa aina mbalimbali ni wa kutosha.

Bodi inaweza kukutana kwa ajili ya kufanya shughuli, kuahirisha na vinginevyo kudhibiti mikutano yake itakavyoona inafaa. Mikutano ya bodi inafanyika mara kwa mara kupitia mkakati, ufanisi wa kiuendeshaji na kifedha, na vilevile usimamizi. Mikutano maalum ya bodi inaweza kufanyika wakati itakapohitajika.

Kamati ya Uteuzi hufanya mapitio ya utaratibu wa mwendelezo wa majukumu ya bodi na kamati zake ili kuhakikisha kuwa zina watu sahihi wenye ujuzi na uzoefu kwa siku zijazo. Mkurugenzi Mtendaji ana wajibu wa kuhakikisha kuwa wajumbe wa kamati ya uongozi wana ujuzi, mamlaka na rasilimali za kutosha kutekeleza mkakati wa kampuni.

Uwajibikaji

Bodi ina wajibu wa kuhakikisha kampuni inakuwa na mafanikio. Kazi yake ni kuongoza na kutoa maamuzi ya busara katika kueleleza kampuni kufanikisha ukuaji endelevu na kufanya kazi kwa maslahi ya wanahisa.

Muundo ufuatao unaonesha safu ya viongozi wa Vodacom Tanzania tarehe 31 Machi 2024:

Bodi

Kamati za Bodi

- ▷ Kamati ya Ujira
- ▷ Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji
- ▷ Kamati ya Uteuzi



Mkurugenzi Mtendaji

Kamati ya Utendaji

- ▷ Masuala ya Mahusiano na Taasisi ya Vodacom
- ▷ Fedha
- ▷ Huduma kwa Wateja
- ▷ TEHAMA
- ▷ Kitengo cha Biashara: Wateja wa Biashara
- ▷ Kitengo cha Biashara – Wateja Binafsi
- ▷ Sheria na Udhibiti
- ▷ Huduma za Digitali
- ▷ Kitengo cha Biashara: M-Pesa
- ▷ Dharura na Utekelezaji
- ▷ Mtandao
- ▷ Rasilimali Watu





Kwa mujibu wa utendaji bora, Mwenyekiti na Mkurugenzi mtendaji wana majukumu tofauti. Mwenyekiti ana wajibu wa kuongoza Bodi, wakati Mkurugenzi Mtendaji anawajibika kusimamia uendeshaji wa kampuni.

Katiba ya Bodi inaeleza wajibu wa Bodi, ambao ni pamoja na:



Kufanya uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji na Mkurugenzi wa Fedha



Kusimamia kwa karibu mwelekeo wa kimkakati wa kampuni



Kupitisha miradi mikubwa, ununuzi au mauzo ya vitu



Kufanya uamuzi wa busara kuhusu masuala ya biashara ya kampuni, mbali na menejimenti



Kuhakikisha kuwa miundo, sera na taratibu stahiki zinakuwepo



Kuhakikisha udhibiti wa ndani wa kampuni unakuwa na mafanikio



Kupitia na kutathmini dharura za kampuni



Kupitisha bajeti ya mwaka na mpango wa utekelezaji



Kupitisha matokeo ya pamoja ya fedha ya mwaka na ya muda na vilevile mawasiliano kwenda kwa wadau



Kupitisha muundo wa uongozi na mpango wa mwendelezo wa uwepo wa viongozi; na



Usimamizi wa teknolojia ya habari

Wakurugenzi

Katiba ya kampuni inaeleza kuwa wakurugenzi wanapaswa kustaafu kwa zamu na wanaweza kuchaguliwa tena baada ya kila miaka mitatu.

Mwenyekiti

Katiba inaitaka Bodi kumchagua Mwenyekiti kila mwaka. Bodi ilimchagua tena Jaji (mstaafu) Thomas B. Mihayo kuwa Mwenyekiti kuanzia Novemba 2023. Bodi imeridhia kwamba Mwenyekiti anaweza kutekeleza majukumu ya nafasi hii ipasavyo. Katika maadhimisho ya kuchaguliwa kwake, Bodi itajadili uteuzi wa kushika nafasi hiyo.

Kupata ushauri huru

Bodi inatambua kuwa inawezekana kukawa na wakati ambapo wakurugenzi wakaona kuwa ni muhimu kupata ushauri huru wa kitaalamu. Kampuni itagharambia huduma hii kwa mujibu wa utaratibu uliopo.


Taarifa ya shughuli za uongozi

Vodacom Tanzania PLC

Mikutano ya Bodi

Jedwali hapo chini linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi katika mikutano ya Bodi kwa mwaka huu:

Jina la Mkurugenzi	Mikutano ya Bodi		Mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji		Mikutano ya Kamati ya Ujira	Mikutano ya Kamati ya Uteuzi	Jumla mahudhurio
	Robo mwaka	Maalum	Robo mwaka	Maalum			
Jaji (Mstaafu) Thomas B Mihayo (Mwenyekiti)	4/4	7/7				2/2	13/13
Bi Margaret Ikongo	4/4	7/7	4/4	4/4			19/19
Bi Thembeka Semane	4/4	6/7	4/4	3/4			17/19
Bi Kanini Mutooni	4/4	5/7	4/4	3/4	3/3	2/2	21/24
Bi Raisibe Morathi	3/4	6/7					9/11
Bw Nkateko Nyoka	4/4	7/7					11/11
Bw Diego Gutierrez	3/4	7/7			2/3		12/14
Bw Matimba Mbungela	4/4	6/7			3/3	2/2	15/16
Bw Sudhersan Ramasamy	4/4	7/7					11/11
Bw Sitholizwe Mdlalose	2/4	4/7					6/11
Bw Philip Besimire	4/4	7/7					11/11
Bi Hilda Bujiku	4/4	7/7					11/11
Jumla	91.7%	90.5%	100.0%	83.3%	88.9%	100.0%	91.2%




M-Pesa Limited

Mikutano ya Bodi ya M-Pesa Limited

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi kwenye mikutano ya Bodi ya M-Pesa Limited mwaka huu:

Jina la Mkurugenzi	Mikutano ya Bodi		Mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji		Jumla Mahudhurio
	Robo mwaka	Maalum	Robo mwaka	Maalum	
Bw Sitoyo Lopokoiyit (Mwenyekiti)	3/4	1/1			4/5
Bw Epimack Mbeteni	2/4	0/1			2/5
Bw Olaf Mumburi	4/4	1/1	4/4	1/1	10/10
Bi Hilda Bujiku	4/4	1/1	4/4	1/1	10/10
Bw Philip Besiimire	3/4	0/1			3/5
Jumla	80.0%	60.0%	100%	100.0%	82.9%

Jinsia



Miaka

40 – 49

5

Mahudhurio ya vikao vya bodi

82.9%

Muundo wa Bodi



Muda waliohudumu kwenye nafasi hizi



Taarifa ya masuala ya ujira

Barua kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira:

Ni heshima kubwa kwangu kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira mwaka huu. Tangu nilipojiunga na Bodi ya Vodacom, nimevutiwa na falsafa ya ujira ya Kampuni na utekelezaji wake, pamoja na uwazi uliopo juu ya masuala ya ujira.

Kanini Mutooni

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira



Dhumuni kuu la sera ya ujira ya Vodacom ni kuhakikisha kwamba motisha za muda mfupi na muda mrefu zinahimiza na kutunza utekelezaji mzuri wa azma, dhamira, na mkakati wa Vodacom, ili kuiwezesha Kampuni kupata matokeo chanya ya muda mrefu. Aidha, Kampuni inaweka mkazo katika ushirikishwaji wa wafanyakazi na kuwawezesha kupata manufaa mengineyo mahali pa kazi, mbali na malipo ya kifedha.

Nimevutiwa na jinsi Kampuni inavyochagua manufaa haya – ambalo sio zoezi la kuweka alama tu, bali manufaa haya yameundwa kuendana na mahitaji ya kila mfanyakazi. Haya yote yamepelekea ari chanya ndani ya Vodacom, na kuwezesha kudumisha nafasi yake ya uongozi ndani ya kundi la makampuni ya Vodafone kwenye kipimo cha Ari ya Timu na Ushirikishwaji wa Wafanyakazi.

Mwaka huu, tulielekeza mkazo mkubwa katika kukuza usawa wa kijinsia na uwiano sahihi wa kazi na maisha binafsi, huku tukitambua nafasi ya kila mtu, yaani – wanawake na wanaume katika kufikia uwiano huu. Mbali na mipango ya muda mrefu inayowalenga wanawake, mwaka huu Kampuni pia iliandaa midahalo ya wanaume ili washiriki katika kutoa mitazamo yao juu ya uwiano kati ya kazi na maisha binafsi, hivyo kukuza ushirikishwaji kwa wote. Kipaumbele chetu kingine kimekuwa ni kutoa mafunzo ya awali kwa Bodi ya Wakurugenzi juu ya masuala ya mazingira, jamii na utawala, ambazo ni nguzo muhimu zinazoisadia Vodacom kutimiza azma na wajibu wake kwa jamii.

Huu ni wakati bora kwa Kampuni kwa kuwa, uchumi wa ndani unazidi kuimarika na, kumekua na ongezeko maradufu la fursa mbalimbali za ukuaji katika sekta ya mawasiliano. Hata hivyo, tunatambua, ushindani uliopo katika ujuzi wa kiufundi na kiuongozi, huku benki na kampuni chipukizi zikiajiri sana

wajuzi hao kutoka sekta yetu. Kwa kuzingatia muktadha huu, ni muhimu kuwa na motisha za kutosha kwa wajuzi wetu, ikisaidiwa na utamaduni mzuri mahali pa kazi, ili kuhakikisha tunaendelea kuvutia na kubakiza vipaji bora, watakaoiwezesha Kampuni kuendeleza nafasi ya uongozi katika sokoni. Kama ilivyoelezwa katika taarifa hii, ninaamini kwamba Kampuni inatoa ujira ulio sawa na stahiki ambao utavutia, kubakiza na kutoa motisha kwa watendaji wenye uwezo wa hali ya juu, waliopewa jukumu la uongozi kwa maslahi bora ya muda mrefu ya Kampuni.

Katika kuandaa taarifa hii, kamati imezingatia miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana ('CMSA'), 1994. Tumeridhika kwamba taarifa inaafikiana na miongozo ya utawala bora kwa kampuni zilizoordheshwa kwenye soko la hisa nchini Tanzania, huku tukiwa waangalifu juu ya taarifa za mtu binafsi au taarifa nyeti za soko. Ninakuhimiza usome taarifa hii na kutoa maoni yoyote juu ya falsafa na sera ya ujira ya Kampuni.

Mwisho, ningependa kushukuru wenzangu kwenye Kamati ya Ujira kwa mchango wao mkubwa mwaka huu.

Kanini Mutooni
Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira
17 Julai 2024

Kulingana na miongozo ya Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana kuhusu taratibu za usimamizi wa makampuni ya umma yaliyoordheshwa nchini Tanzania, taarifa hii inaeleza sera za Vodacom Tanzania za ujira kwa wakurugenzi watendaji na wakurugenzi wasio watendaji hususan kiasi na aina za ujira kwa wakurugenzi ikiwa ni pamoja na wakurugenzi wasio watendaji kwa pamoja.

Falsafa, sera na mfumo wetu wa ujira kwa mwaka huu kwa wakurugenzi watendaji. Lengo letu ni kuwavutia, kuwawezesha kubaki na kuwapatia motisha watendaji wenye uwezo wa hali ya juu, sambamba na kulinganisha ujira wao na maslahi ya wanahisa na taratibu bora za utekelezaji.

Utaratibu wetu wa stahiki za ajira ni mpana, wenye ulinganifu kwenye vipengele vifuatavyo:

- ▷ Ujira wa uhakika (GP);
- ▷ Motisha ya muda mfupi (STIP);
- ▷ Motisha ya muda mrefu (LTIP);
- ▷ Programu mbalimbali za utambuzi;
- ▷ Fursa mbalimbali za kujifunza na kujiendeleza;
- ▷ Mazingira ya kazi yanayovutia; na
- ▷ Programu nzuri ya ustawi wa wafanyakazi.

Viongozi watendaji wanafuata falsafa ya 'Jumla ya gharama kwa kampuni', ambayo tunairejelea kama ujira uhakika (GP). Michango katika huduma za tiba, fedha za ustaafu na mafao ya bima yamejumuishwa katika GP.

Vipengele hivyo hapo juu vinaendana na kuimarishwa kwa utaratibu wetu wa kutathmini utendaji kazi na kuendeleza vipaji. Sera yetu ni kuwapa marupurupu viongozi wetu watendaji kutokana na michango yao katika ufanisi wetu kimkakati, kifedha na kiutendaji. Ili kuwa muajiri anayeheshimika katika sekta yetu tunahitaji kuvutia, kuendeleza na kubakiza vipaji bora na rasilimali ya wataalamu wa ndani na kimataifa.

Kila mwaka tunalinganisha viwango na kuongeza malipo katika GP kulingana na soko, ufanisi binafsi na uwezo. Tathmini ya ufanisi binafsi na uwezo wa kiutendaji hubainishwa kupitia utaratibu wetu wa kupima utendaji na uwezo wa kiutendaji wa wafanyakazi wetu. Matokeo ya utaratibu huu, huchangia katika uamuzi wa mabadiliko ya motisha ya muda mfupi na muda mrefu.

Kiasi hiki ni jumla ya ada kwa dola ya Marekani, ikijumuisha kodi zote pamoja na kodi ya zuo, inayolipwa kwa shilingi ya Kitanzania kwa wakurugenzi wazawa, randi ya Afrika Kusini kwa wakurugenzi wakazi wa Afrika Kusini na dola ya Marekani kwa wakurugenzi wengine. Ada hii inalipwa kila robo mwaka.

Motisha yetu ya muda mfupi inayolipwa kama bonasi ya fedha taslimu hutokana na kufikia malengo kwenye utendaji wa masuala ya fedha, mikakati, uendeshaji wa vitengo na malengo binafsi ambayo kila mtendaji amepewa. Kiasi kilichopo kwa ajili ya motisha ya muda mfupi kinatokana na utendaji kwenye masuala ya fedha kadiri ya malengo yaliyowekwa na kukubaliwa.

Viongozi watendaji ambao wametumwa kufanya kazi Vodacom Tanzania kutoka Vodacom Group Limited, hulipwa motisha ya muda mrefu kwa mujibu wa taratibu za Vodacom Group Limited, ambapo hupewa umiliki wa hisa na mwajiri wao. Hii huchochea utendaji unaoakisi umiliki na uaminifu, na huchangia katika lengo la Vodacom la kuwabakiza watendaji hodari. Mfumo huo ni mfumo kamili wa umiliki, na matokeo yake wahusika hupata gawio kutoka siku walipopewa hisa japokuwa thamani ya hisa inaweza tu kupatikana baada ya miaka mitatu na ni kwa kulingana na kiwango ambacho masharti ya kupewa hisa hizo yametimizwa.

Taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji

Ujira wa wakurugenzi watendaji – Malipo ya Uhakika

Ujira wa wakurugenzi watendaji ulifanyiwa mapitio kwa kuzingatia ulinganishi na ujira wa watendaji wengine katika soko, na pia athari za kushindwa kuwabakiza watendaji muhimu katika menejimenti.

Kwa kuzingatia utaratibu/sera ya ujira, taarifa iliyo kwenye toleo hili ni kwa wakurugenzi waliostahili, ambapo maamuzi yote yanayohusu ujira yamefanyika kwa kuzingatia utaratibu wa ujira na kuidhinishwa na wanahisa. Kama ilivyo kwa mwaka uliotangulia, hakuna mabadiliko yaliyofanywa katika utekelezaji wa sera/utaratibu wa ujira katika mwaka huu.

Taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji zimetolewa kwa muhtasari katika jedwali hapo chini na pia zimewasilishwa katika Maelezo 35 katika taarifa za pamoja za fedha na taarifa binafsi za fedha za kampuni (nakala ya kiingereza) yaliyopo katika ukurasa wa 124.

Wakurugenzi	Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji					Jumla
	Bodi	Utekelezaji	Ujira	Uteuzi		
TB Mihayo	150 000					150 000
M Ikongo	30 000	15 000				45 000
K Mutooni	30 000	8 000	12 000	3 000		53 000
T Semane	30 000	8 000				38 000
D Gutierrez	30 000		4 000			34 000
M Mbungela	30 000		4 000	3 000		37 000
N Nyoka	30 000					30 000
S Mdalose	30 000					30 000
S Ramasamy	30 000					30 000
R Morathi	30 000					30 000
H Bujiku						–
P Besiimire						–
						477 000



Taarifa ya Mkutano Mkuu

Vodacom Tanzania Public Limited Company

(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
(Namba ya usajili 38501)
(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)
(‘Vodacom Tanzania’ au ‘Kampuni’)

Taarifa inatolewa kuwa, mkutano mkuu wa nane wa Kampuni kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024 utafanyika kwa njia ya kielektroniki siku ya Jumatano tarehe 11 Septemba 2024 kuanzia saa nne asubuhi. Mkutano huu utajadili yafuatayo:

1. Kuthibitisha kumbukumbu

Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa saba uliofanyika tarehe 22 Septemba 2023.

Azimio la kawaida namba 1

“ILIAMULIWA KUWA kumbukumbu za mkutano mkuu wa saba uliofanyika tarehe 22 Septemba 2023 zimethibitishwa.”

Nakala za kumbukumbu zinapatikana kwenye tovuti ya Kampuni www.vodacom.co.tz/annual-general-meeting.

2. Kupitisha taarifa za fedha za mwaka zilizokaguliwa

Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024.

Azimio la kawaida namba 2

“ILIAMULIWA KUWA taarifa za fedha zilizokaguliwa za Kampuni, pamoja na taarifa ya wakaguzi huru na ya wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024, zimepokelewa na kupitishwa.”

Nakala za taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024 zinapatikana katika tovuti ya Kampuni www.vodacom.co.tz/financials.

3. Uchaguzi wa wakurugenzi

Kwa kupitia maazimio tofauti:

- Bw Dejan Kastelic aliteuliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji kwa mujibu wa ibara ya 86 ya Katiba ya Kampuni, kujaza nafasi iliyojitokeza katika Bodi na kuendelea kutekeleza majukumu ya kiofisi hadi mkutano wa kawaida unaofuata, na hivyo anastahili kuchaguliwa. Wasifu wake upo ukurasa wa 35.
- Bw Haytham Ammar aliteuliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji kwa mujibu wa ibara ya 86 ya Katiba ya Kampuni, kujaza nafasi iliyojitokeza katika Bodi na kuendelea kutekeleza majukumu ya kiofisi hadi mkutano wa kawaida unaofuata, na hivyo anastahili kuchaguliwa. Wasifu wake upo ukurasa wa 35.
- Bw Matimba Mbungela, Bw Diego Gutierrez and Bi Raisibe Morathi wanapaswa kustaafu katika mkutano huu kwa mujibu wa ibara 104 na 105 za Katiba ya Kampuni. Ibara hizo zinabainisha kuwa licha ya kustaafu, wanaweza kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa wakurugenzi. Wasifu wao upo ukurasa wa 35.

Azimio la kawaida namba 3

“ILIAMULIWA KUWA Bw Dejan Kastelic amechaguliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji.”

Azimio la kawaida namba 4

“ILIAMULIWA KUWA Bw Haytham Ammar amechaguliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji.”

Azimio la kawaida namba 5

“ILIAMULIWA KUWA Bw Matimba Mbungela amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi asiye mtendaji.”

Taarifa ya Mkutano Mkuu inaendelea

Azimio la kawaida namba 6

"ILIAMULIWA KUWA Bw Diego Gutierrez amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

Azimio la kawaida namba 7

"ILIAMULIWA KUWA Bi Raisibe Morathi amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

4. Uteuzi wa Ernst & Young kuwa wakaguzi huru wa Kampuni

Kuteua kampuni ya Ernst & Young Inc., kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji, kuwa wakaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka.

Azimio la kawaida namba 8

"ILIAMULIWA KUWA Ernst & Young Inc. imeteuliwa kuwa mkaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka."

5. Uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

Kupitia maazimio tofauti na kwa mujibu wa kifungu cha 32(f) cha Katiba ya Kampuni, Bi Margaret Ikongo, Bi Thembeke Semane na Bi Kanini Mutooni wakiwa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji wachaguliwa kuendelea kuwa wajumbe. Wasifu wao upo ukurasa wa 35.

Azimio la kawaida namba 9

"ILIAMULIWA KUWA Bi Margaret Ikongo amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

Azimio la kawaida namba 10

"ILIAMULIWA KUWA Bi Thembeke Semane amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

Azimio la kawaida namba 11

"ILIAMULIWA KUWA Bi Kanini Mutooni amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

6. Gawio

Kuidhinisha gawio la mwisho la Shi 11.93 kwa kila hisa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2024 kama ilivyopendekezwa na wakurugenzi. Gawio litalipwa kabla au Jumatano ya tarehe 16 Oktoba 2024 kwa wanahisa waliosajiliwa kwenye kitabu cha usajili baada ya kufunga biashara ya hisa tarehe 15 Agosti 2024.

Azimio la kawaida namba 12

"ILIAMULIWA KUWA gawio la Shi 11.93 kwa hisa ya kawaida kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2024 limeidhinishwa."

7. Ada ya wakurugenzi

Kuidhinisha ada ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 477 000 hadi hitimisho la mkutano mkuu ujao wa mwaka, ili kuiwezesha Kampuni kuwavutia watu wenye uwezo, ujuzi na uzoefu unaotakiwa ili kutoa mchango unaofaa kwa Kampuni. Hakuna mapendekezo ya mabadiliko ya ada.

Azimio la kawaida namba 13

"ILIAMULIWA KUWA kiwango cha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji cha dola za Kimarekani 477 000 kimeidhinishwa kwa mchanganuo ufuatao:

	Pendekezo la ada Dola ya Marekani ¹	Ada ya sasa Dola ya Marekani
Mwenyekiti wa Bodi	150 000	150 000
Mjumbe wa Bodi	30 000	30 000
Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji	15 000	15 000
Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji	8 000	8 000
Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira	12 000	12 000
Mjumbe wa Kamati ya Ujira	4 000	4 000
Mjumbe wa Kamati ya Uteuzi	3 000	3 000

1. Ada hii inajumuisha kodi zote ikijumuisha kodi ya zuio, inayolipwa kwa shilingi ya Kitanzania kwa wakurugenzi wazawa, randi ya Afrika Kusini kwa wakurugenzi wa Afrika Kusini na dola ya Marekani kwa wakurugenzi wengine. Ada hii inalipwa kila robo mwaka.

Wasifu wa Wajumbe wa Bodi

Dejan Kastelic (43)

Mkurugenzi asiye mtendaji

Shahada ya Sayansi katika Uhandisi Umeme kutoka Chuo kikuu cha Maribo kilichopo Slovenia; Alisoma Chuo Kikuu cha Harvard kilichoko Boston Marekani na INSEAD

Bw. Kastelic aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Teknolojia wa Vodacom Group, Afrika Kusini mwezi Agosti 2020. Kabla ya kujiunga na Vodacom, alikuwa Afisa Mkuu wa Teknolojia na Habari katika kampuni ya PT Indosat Ooredoo TBK, sehemu ya kampuni ya Kundi la makampuni ya Ooredoo huko Qatar. Aidha, aliwahi kuwa Mkurugenzi wa kampuni ya Indosat, Singapore na ni Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi wa Posta Slovenije d.o.o. Bw. Kastelic alianza kazi katika kampuni ya simu Amis Ltd hadi kufikia nafasi ya Afisa Mkuu wa Teknolojia. Mwaka 2009 aliamia kampuni ya IBM Ulaya Mashariki na Kati kama Meneja Usimamizi wa Rasilimali. Mwaka 2012 alijiunga na kampuni ya Telkom Austria akiwa kama Mkurugenzi Mtendaji na Afisa Mkuu wa Teknolojia na Habari na baadaye akawa Mkurugenzi wa Kundi na Afisa Mkuu wa Teknolojia na Habari akisimamia kampuni za simu – Vip mobile, Serbia na Si.Mobil Slovenia. Mwaka 2015, aliamishwa kampuni ya Mobilnet Bulgaria hadi alipoteuliwa kwenye nafasi aliyoishikilia mwanzo katika kampuni ya Indosat. Bw. Kastelic pia ni mkurugenzi wa bodi ya Vodacom Msumbiji na Vodacom Lesotho.

Haytham Ammar (42)

Mkurugenzi asiye mtendaji

Shahada ya Uhasibu na Usimamizi wa Biashara, Cheti cha Taaluma ya Uhasibu

Haytham aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Fedha wa Makampuni Tanzu ya Vodacom mwezi Juni 2024. Kabla ya kujiunga na Vodacom, alikuwa Afisa Mkuu wa Fedha wa M-Pesa Africa. Aidha, aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Fedha wa Vodafone Ghana ambapo alitoa mchango mkubwa katika kufanya mageuzi ya kibashara yaliyopelekea ukuaji kiendeshaji na kifedha huku akichochea ongezeko la thamani ya biashara kulingana na rasilimali chache zilizokuwepo. Anasifiwa pia kwa kuboresha mazingira ya uhibitaji wa mapato, ugavi, usimamizi wa madeni, na uwasilishaji wa taarifa za kifedha. Haytham alianza kufanya kazi na Vodacom mwaka wa 2007 alipojiunga na Vodafone Misri, ambapo majukumu yake yalikusishwa nyanja mbalimbali ikiwemo Mipango ya Fedha, Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha, na Mipango Maamuzi, akiisaidia timu ya Misri katika kupanga na kutekeleza mipango mikakati muhimu kama vile ujenzi wa minara ya teknolojia ya 4G, maboresho ya kidigitali, na kuchochea ufanisi katika gharama za matumizi.

Raisibe Morathi (55)

Mkurugenzi asiye mtendaji

Shahada ya Uzamili ya Filosofa, Stashahada ya juu ya masuala ya kodi kutoka Chuo Kikuu cha Wits, Mhitimu wa programu ya menejimenti ya INSEAD (Ufaransa), Cheti cha Taaluma ya Uhasibu ya Afrika Kusini (CA, SA)

Raisibe aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Fedha wa Vodacom Group Limited mwezi Novemba 2020. Alijiunga na Vodacom akitokea Nedbank Group ambapo alikuwa Afisa Mkuu wa Fedha tangu Septemba 2009. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 27 katika huduma za fedha katika mashirika mbalimbali makubwa huko Afrika Kusini, ikiwa ni pamoja na Nedbank Group, Sanlam Group na Industrial Development Corporation. Raisibe pia ni mkurugenzi asiye mtendaji wa bodi za Vodacom Afrika Kusini na Safaricom PLC.

Diego Gutierrez (48)

Mkurugenzi asiye mtendaji

Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara na Masoko, Chuo Kikuu cha Católica, Bolivia

Diego aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Uendeshaji wa Vodacom International Business mwezi Agosti 2017. Diego ana uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika shughuli za kimataifa katika sekta ya mawasiliano ya simu hususan kwenye masoko yanayoibukia huko Latini Amerika, Afrika na visiwa vya Karibi. Ana uzoefu uliohibitika wa kufanya mageuzi ya kibashara na kuwezesha ongezeko la ufanisi wa uendeshaji, kupitisha makampuni katika vipindi vigumu vya mabadiliko na kutafisiri mikakati ya mashirika kuwa matokeo ya uendeshaji yanayoonekana. Bw. Gutierrez pia ni mkurugenzi wa bodi ya Vodacom Congo DRC, Vodacom Lesotho, Vodacom Msumbiji, M-Pesa Africa na M-Pesa Africa Kusini.

Matimba Mbungela (52)

Mkurugenzi asiye mtendaji

Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Kwazulu Natal, Shahada ya Utawala, Chuo Kikuu cha Venda, Stashahada ya Juu ya Rasilimali watu, Chuo Kikuu cha Cape Town, Mhitimu wa Programu ya Vodafone kwenye ubora wa masuala ya rasilimali watu

Matimba aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa Vodacom Group Limited mwezi April 2014. Kabla ya kushika nafasi hii, alikuwa Afisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa Vodacom South Africa hadi Aprili 2014. Matimba amefanya kazi ndani ya Vodacom/Vodafone Group tangu 2003 akishikilia nafasi mbalimbali katika Kitengo cha Rasilimali watu. Kwa miaka mitatu alifanya kazi Vodafone kama Mkuu wa Kanda ya Afrika, Mashariki ya Kati na Asia Pasifiki “AMAP” akihusika na Ufanisi na Mabadiliko na pia kama Mkuu wa Vipaji wa Kanda. Kabla ya hapo alikuwa anashughulikia Usimamizi wa Vipaji katika Vodacom kwa miaka sita ambapo alitekeleza kwa mafanikio kujumuishwa kwa mkakati wa vipaji katika mkakati wa dunia wa Vodafone. Uzoefu wake wa siku za nyuma ni pamoja na kufanya kazi za Afisa Rasilimali watu katika kampuni za BMW Afrika Kusini na Unilever. Matimba anawakilisha Vodacom Employee Trust (‘Siyanda’) katika Bodi ya YeboYethu, pia ni Mkurugenzi Asiye Mtendaji wa Vodacom Msumbiji na Vodacom Lesotho na ni mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Unisa GSBL.

Margaret Ikongo (66)

Mkurugenzi huru

Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii

Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu Huria, Tanzania. Cheti cha Kimataifa cha Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Taasisi ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Uingereza. Diploma ya Kimataifa ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi na Mjumbe Mhitimu wa Taasisi ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Uingereza. Mwanachama katika Taasisi ya masuala ya Bima, Uingereza

Margaret aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Pia ni mjumbe wa bodi ya wakurugenzi ya Actuarial and Risk Consulting na Metrolife and Meticulus Insurance. Kabla ya hapo, Margaret alikaa kwenye Bodi ya benki ya NMB na AAR Insurance Tanzania, pamoja na Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Margaret ana uzoefu mkubwa katika masuala ya fedha na utawala bora akiwa ameupata kutokana na kufanya kazi katika sekta ya bima ambapo alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa kwa kupindi cha miaka kumi. Margaret pia alikuwa mshauri wa Kamishna wa Mamlaka ya Uhibitaji wa Bima Tanzania pamoja na Kaimu Mkuu wa Kurugenzi ya Ufundi.

Taarifa ya Mkutano Mkuu inaendelea

Thembeke Semane (48)

Mkurugenzi huru

Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii

Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Monash; Stashahada ya Juu katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Biashara cha Pretoria Gordon; Shahada ya Biashara katika Uhasibu; Chuo Kikuu cha Transkei (Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Walter Sisulu kwa sasa); Mwanachama wa Taasisi ya Taaluma ya Benki ya Afrika Kusini

Thembeke aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Thembeke ana uzoefu katika masuala ya biashara ukihusisha mikakati ya mashirika, utekelezaji wa mifumo ya biashara, miradi yenye thamani kubwa, utekelezaji na ufuatiliaji, utawala bora na vilevile usimamizi wa fedha. Thembeke ni mkurugenzi wa Linea Consulting (Pty) Ltd, mjumbe wa Kamati ya Udhhibiti ya ACASA & ATNS, akiripoti kwa Waziri wa Usafirishaji wa Afrika Kusini na pia, ni mjumbe wa Baraza la ICASA. Thembeke anafanya kazi kama mjumbe wa bodi wa Idara ya Makazi EAAB, ambapo ni Mwenyekiti wa Kamati yake ya Fedha na Uwekezaji na pia, ni mjumbe wa Kamati za Ukaguzi na Dharura pamoja na ya Rasilimali watu na Ujira. Pia, Thembeke ni mjumbe wa bodi na mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Dharura na Kamati ya Ujira ya Mamlaka ya usimamizi wa Mbuga za Wanyama za Afrika Kusini. Vilevile, Thembeke ni mjumbe wa South African Heritage Resource Agency na Kamati ya Uthibiti na Usimamizi wa Utendaji wa Manispaa ya Sol Plaatje.

Kanini Mutooni (48)

Mkurugenzi huru

Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii

Elimu ya utekelezaji wa Sera za Kimataifa, Shule ya masuala ya kiserikali ya Harvard. Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Shule ya Biashara Cass ya Chuo Kikuu cha Jiji la London. Diploma ya masuala ya Dhamana (Uingereza). Cheti cha Taaluma ya Usimamizi katika Uwekezaji (Uingereza). Cheti cha Taaluma ya Uhasibu (ACCA), Uingereza. Shahada ya Biashara, Chuo Kikuu cha Kikatomliki, Kenya


Kanini aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Oktoba 2022. Kanini ni Mkurugenzi Mtendaji wa Draper Richards Kaplan Foundation kwa Afrika. Hivi sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Draper Richards Kaplan Foundation akisimamia Afrika. Pia ni mjumbe katika Bodi za Financial Sector Deepening Africa (FSDA); MCE Social Capital, the United Nations Capital Development Fund, Africa Enterprise Challenge Fund, Amref Health Innovation na CDC UK PLC. Kabla ya hapo, Kanini alikuwa mjumbe wa Bodi katika benki za uwekezaji huko Uingereza na Marekani ikiwa ni pamoja na Bank of America-Merrill Lynch na Dresdner Kleinwort Benson.

Tarehe ya kufunga rejesta

Tarehe ya kufunga rejesta ya wanahisa wa Kampuni kwa madhumuni ya kustahili kuhudhuria, kushiriki na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni Jumatano 4 Septemba 2024.

Ushiriki kwa njia ya kielektroniki

Mkutano mkuu wa mwaka utafanyika kwa njia ya kielektroniki kama ilivyoainishwa kwenye kifungu 29 na 63 cha Katiba ya Kampuni. Wanahisa waliosajiliwa kwenye rejesta hadi kufikia tarehe ya kufunga rejesta hiyo, watapokea ujumbe mfupi wa maneno wenye taarifa za kuwawezesha kuingia kwenye mkutano huo. Mkutano mkuu wa mwaka utaooneshwa mubashara kupitia kiunga cha wavuti kwenye vifaa janja vilivyounishwa na intaneti.

 Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya Kampuni www.vodacom.co.tz/annual-general-meeting

Wanahisa watawajibika kwa gharama za data na mtandao. Kampuni haitawajibika na upotevu wa mawasiliano kutokana na matatizo ya kimtandao/kuishiwa muda wa hewani/kukatika kwa umeme/na matatizo ya kiufundi ya kielektroniki yanayoweza kuathiri ushiriki wa mwanahisa kwenye mkutano mkuu mwaka kwa njia ya mtandao.

Wanahisa wanahimizwa kutuma maswali yatokanayo na maazimio yaliyopo kwenye taarifa hii kabla ya mkutano mkuu kwenda kwenye barua pepe investorrelations@vodacom.co.tz kabla ya Ijumaa ya tarehe 6 Septemba 2024 saa 4:00 asubuhi. Majibu ya maswali hayo yatatolewa katika mkutano mkuu. Uwasilishaji wa maswali haumzui mwanahisa kuuliza maswali siku ya mkutano mkuu.

Mahudhurio

Wanaostahili kuhudhuria, kuzungumza na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni wanahisa tu.

Wanahisa wanaweza kuteua wawakilishi kuhudhuria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yao. Mwakilishi si lazima awe mwanahisa wa Kampuni. Fomu ya uwakilishi iliyojazwa, inayopatikana kwenye tovuti ya Kampuni, pamoja na risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, kitambulisho cha taifa/kura/leseni ya udereva na taarifa za mawasiliano vitumwe kwa barua pepe kwenda investorrelations@vodacom.co.tz au viwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni, ghorofa ya 15, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4:00 asubuhi Ijumaa ya tarehe 6 Septemba 2024. Kujazwa kwa fomu ya mwakilishi hakumzui mwanahisa yeyote kuhudhuria mkutano mkuu wa mwaka.

Upigaji kura utaendeshwa kulingana na Katiba na kanuni za Kampuni. Maazimio ya kawaida yatakayopitishwa katika mkutano mkuu huu yatapasa kuungwa mkono na zaidi ya 50% ya kura za wanahisa. Azimio maalum litapaswa kuungwa mkono na angalau 75% ya kura za wanahisa.

Wanahisa wenye hisa zisizo kwa majina yao lazima wawapatie watunzaji au wawakilishi wao maelekezo ya kupiga kura katika mkutano mkuu wa mwaka. Kama mtunzaji au mwakilishi wako hatapokea maelekezo kutoka kwako, kama itakavyokuwa, itabidi kufanya maamuzi kulingana na mamlaka uliyoatoa wake.

Wanahisa wanahimizwa kuendelea kufuatilia tovuti ya Kampuni ili kupata taarifa zaidi zinazohusiana na mkutano mkuu wa mwaka.

Imeidhinishwa na Bodi.



Caroline M Mduma
Katibu wa Kampuni
19 Agosti 2024

Fomu ya Mwakilishi

Vodacom Tanzania Public Limited Company

(Imesajiliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

(Namba ya Usajili 38501)

(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)

("Vodacom" au "Kampuni")

Kifungu A – Ijazwe na wanahisa wote

Jina Kamili

Namba ya hati ya hisa (CDS A/c No)

Idadi ya hisa mwanahisa anazomiliki

Kifungu B – Ijazwe na wanahisa watakaoteuwa wawakilishi (na si Mwenyekiti) kuhudhuria mkutano kwa niaba yao

Mimi(Sisi), mwenye/wenye hati ya hisa zenye idadi ya hisa za kampuni kwa mujibu wa kifungu A, namteua/tunamteua (angalia maelekezo namba 1&2)

au akishindwa yeye,

au akishindwa yeye,

Mwenyekiti Mwenyekiti wa mkutano mkuu wa mwaka kuwa mwakilishi wangu/wetu kuhudhuria, kushiriki mijadala na kupiga kura kwa niaba yangu/yetu katika mkutano mkuu wa mwaka wa sita utakaofanyika kwa nji ya kielektroniki siku ya Jumatano, tarehe 11 Septemba 2024 kwa lengo la kutoa maamuzi na kupitisha maazimio ya kawaida, kupiga kura ya kuafiki au kutokuafiki au kutoshiriki kwenye upigaji kura kulingana na hisa zilizoandikishwa kwa jina langu/letu.

Kifungu C – Ijazwe na wanahisa wote

Weka alama x kwenye kisanduku kulingana na matakwa yako.

Vinginevyo mwakilishi wako atapiga kura atakavyoona inafaa.

	Naafiki	Siafiki	Sishiriki
1. Azimio la kawaida namba 1 Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa mwaka uliofanyika tarehe 22 Septemba 2023			
2. Azimio la kawaida namba 2 Kupitisha taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024			
3. Azimio la kawaida namba 3 Kumchagua Dejan Kastelic kuwa mkurugenzi asiye mtendaji			
4. Azimio la kawaida namba 4 Kumchagua Haytham Ammar kuwa mkurugenzi asiye mtendaji			
5. Azimio la kawaida namba 5 Kumchagua tena Matimba Mbungela kuwa mkurugenzi asiye mtendaji			
6. Azimio la kawaida namba 6 Kumchagua tena Diego Gutierrez kuwa mkurugenzi asiye mtendaji			
7. Azimio la kawaida namba 7 Kumchagua tena Raisibe Morathi kuwa mkurugenzi asiye mtendaji			
8. Azimio la kawaida number 8 Kuchagua Ernst & Young Inc. kuwa wakaguzi wa Kampuni kwa mwaka unaoishia Machi 2025			
9. Azimio la kawaida namba 9 Kumchagua tena Margaret Ikongo kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji			
10. Azimio la kawaida namba 10 Kumchagua tena Thembeke Semane kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji			
11. Azimio la kawaida namba 11 Kumchagua tena Kanini Mutooni kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji			
12. Azimio la kawaida namba 12 Kuidhinisha gawio la shilingi 11.93 kwa hisa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024			
13. Azimio la kawaida namba 13 Kuidhinisha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 477 000 kwa mwaka			

Imetiwa sahihi tarehe

mwezi Septemba 2024

Sahihi:

Sahihi:

Fomu ya mwakilishi iliyojazwa iwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni ya Vodacom Tanzania PLC kabla saa 4 asubuhi, Ijumaa tarehe 6 Septemba 2024.

Maelekezo ya fomu ya mwakilishi

1. Mwanahisa anayepaswa kuhudhuria katika mkutano mkuu anaweza kuteua mwakilishi wake kuhudhuria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yake. Mwakilishi sio lazima awe mwanahisa wa kampuni. Kwa makampuni, fomu ya mwakilishi ijazwe na afisa mwenye mamlaka na iwekwe muhuri wa Kampuni husika.
2. Weka alama 'X' kwenye eneo la kujaza kwenye fomu kulingana na kura unayotaka kupiga katika agenda husika. Iwapo utapenda kupiga kura kwa hisa pungufu ya hisa unazomiliki, onyesha idadi ya hisa pungufu ambazo ungependa zipige kura. Iwapo maelekezo haya hayatazingatiwa, mwakilishi atapiga kura atakavyoona inafaa.
3. Mwanahisa anaweza kuweka jina la mwakilishi/wawakilishi wake kwenye sehemu iliyoonyeshwa kwenye hii fomu bila kufuta kipengele cha kuwakilishwa na "Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa mwaka" kilichopo chini ya sehemu ya kuandika majina ya wawakilishi. Mwanahisa atapaswa kuweka sahihi yake iwapo atafuta kipengele hicho. Mwakilishi ambaye jina lake limejazwa likiwa la kwanza kwenye fomu ya uwakilishi akihudhuria mkutano mkuu ndiye atahusika kufanya maamuzi.
4. Fomu za mwakilishi zilizojazwa pamoja na hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, ziwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni – ghorofa ya 15, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja na 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Jumanne tarehe 6 Septemba 2024. Aidha, fomu zinaweza kusainiwa kisha kuzituma kwa barua pepe ya investorrelations@vodacom.co.tz.
5. Mwanahisa akifanya masahihisho/mabadiliko yoyote kwenye fomu ya mwakilishi, atapaswa kuwekwa sahihi yake pembeni ya masahihisho/mabadiliko hayo.
6. Wenye hisa wenye umri mdogo kisheria wanapaswa kusimamiwa na wazazi/walezi wao ambao watapaswa kuwa na nyaraka za kisheria za kuwathibitisha.
7. Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa mwaka atakubali fomu ya mwakilishi itakavyokuwa imejazwa tofauti na matakwa haya iwapo ataridhika na namna ambavyo mwanahisa atapenda kupiga kura.
8. Kwa wale wenye hisa za pamoja/vikundi:
 - Yeyote kati yao anaweza kutia sahihi kwenye fomu hii
 - Kura ya mwanahisa mkubwa (ukubwa wa hisa utajulikana kulingana na majina yaliorodheshwa kwenye rejista ya wanahisa wa Kampuni) itakayopigwa na yeye binafsi au kutumia mwakilishi, ndio itakayoruhusiwa kwa niaba ya wanahisa wenzake kwenye kikundi.



Bi Caroline Mduma

Katibu wa Kampuni

Ghorofa ya 15, Vodacom Tower, Ursino Estate,
Kiwanja na 23, Barabara ya Bagamoyo,
P.O. Box 2369,
Dar es Salaam
Barua pepe: investorrelations@vodacom.co.tz

Taarifa kuhusu umiliki

Jumla ya hisa	# ya hisa	% ya hisa
Kundi la Makampuni ya Vodacom (Vodacom Group Limited)	1 680 000 200	75.0%
Mfuko wa Pensheni wa Wafanyakazi wa Serikali (Uwekezaji wa Shirika la Umma SOC Limited, Jamhuri ya Afrika Kusini)	164 503 540	7.3%
Wawekezaji wa Kitaasisi (Afrika Mashariki)	252 443 767	11.3%
Wawekezaji wa Kitaasisi (Sehemu nyingine duniani)	48 456 052	2.2%
Wawekezaji wengine	94 596 741	4.2%
	2 240 000 300	100.0%

Umiliki wa hisa kitaasisi	% Umiliki kitaasisi
Tanzania	48.3%
PIC	35.3%
Uganda	6.0%
Wanahisa wengine wa kimataifa	10.4%
	100.0%



Taarifa za Kampuni

Vodacom Tanzania Public Limited Company

(Imeandikishwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

Usajili namba: 38501

(ISIN: TZ1996102715 Share Code: VODA)

Wakurugenzi

TB Mihayo (Mwenyekiti) ¹	M Ikongo ¹
P Besiimire	M Mbungela ⁵
(Mkurugenzi Mtendaji) ²	N Nyoka ⁵
H Bujiku	R Morathi ⁵
(Mkurugenzi wa Fedha) ¹	S Ramasamy ⁶
S Mdlalose ⁵	T Semane ⁵
D Gutierrez ⁴	K Mutooni ⁷

1. Mtanzania 2. Mganda 3. Muingereza 4. Mbolivia
5. Mwafrika Kusini 6. Mhindi 7. Mkenya

Katibu wa Kampuni

Caroline Mduma

Ghorofa ya 15, Vodacom Tower,
Eneo la Ursino, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2369, Dar es Salaam, Tanzania

Ofisi iliyosajiliwa

Ghorofa ya 15, Vodacom Tower,
Eneo la Ursino, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2369,
Dar es Salaam, Tanzania

Mkaguzi wa Hesabu za Fedha

Ernst & Young

EY House
Kiwanja namba 162/1, Barabara ya Mzinga
14111 Oysterbay
S.L.P 2475, Dar es Salaam, Tanzania

Msajili Masuala ya Hisa

CSD & Registry Company Limited

Soko la Hisa la Dar es Salaam
Ghorofa ya 3, Kambarage House
Mtaa wa 6 Ufukoni
S.L.P 70081
Dar es Salaam, Tanzania

Mshauri Mkuu aliyesajiliwa

Orbit Securities Company Limited

Watoa huduma za Kibenki

Citibank Tanzania Limited

Citibank House
Kiwanja namba 1962, Barabara ya Toure, Oysterbay
S.L.P 71625
Dar es Salaam, Tanzania

National Bank of Commerce Limited

Barabara ya Sokoine & Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 1863
Dar es Salaam, Tanzania

NMB Bank Plc

Mtaa wa Ohio /Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P Box 9213
Dar es Salaam, Tanzania

CRDB Bank Plc.

Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 268
Dar es Salaam, Tanzania

Standard Chartered Bank Tanzania

Jengo la International House
Mtaa wa Shaaban Robert/Garden Avenue
S.L.P 9011
Dar es Salaam, Tanzania

Washauri wa Mambo ya Kisheria

IMMMA (Advocates)

Kiwanja namba 357, IMMMA House
Barabara ya Umoja wa Mataifa, Upanga
S.L.P 72484
Dar es Salaam, Tanzania

Lawhill

14112 Regent Estate Mikocheni
Mtaa wa Historia, Kiwanja namba 311
Nyumba namba 96
S.L.P 105646, Dar es Salaam, Tanzania

Mawasiliano ya nje

Zuweina Farah

Mahusiano ya wawekezaji

Albert Maneno
Neema Munuo
investorrelations@vodacom.co.tz
www.vodacom.co.tz/about-us

Dai la haki

Taarifa zisizofuata Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha (‘IFRS’)

Taarifa hii ina baadhi ya hatua zisizofuata Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha ambazo hazijapitiwa au kuripotiwa na wakaguzi wa Kundi la Kampuni za Vodacom (‘Kundi’). Menejimenti ya Kundi inaamini hatua hizi zinatoa taarifa muhimu za ziada kwa kuelewa ufanisi wa Kundi la Vodacom au biashara za Kundi la Vodacom kwa sababu zinaeleza hatua zilizotumiwa na Kundi la Vodacom kutathimini ufanisi. Hata hivyo, taarifa hizi za ziada zilizowasilishwa hazikufasiliwa kwa njia inayofanana na kampuni zote, ikiwa ni pamoja na zile zilizo katika tasnia ya Kundi la Vodacom. Hivyo, inawezekana haiwezi kulinganishwa na hatua zinazofanana na kutolewa taarifa na kampuni nyingine. Kwa kuongezea, ingawa hatua hizi ni muhimu katika usimamizi wa biashara, hazipaswi kuangaliwa kipwekepeke au kama mbadala, badala yake ziwe kama kijalizo, katika hatua za Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha. Rejea katika sehemu ya ‘Ufanisi wetu’ ya taarifa hii kwa maelezo yanayohusiana na mapato ya huduma, EBIT na mapato kwa kila hisa.

Alama za biashara

Vodafone, logo ya Vodafone, M-Pesa, Vodacom, Wakulima Waliunganishwa na Vodafone Supernet ni alama za biashara za Vodafone Group Plc (au ina program zinazosubiria). M-Fundi, M-Shamba, M-Pawa na Vodacom Faraja ni alama za biashara za Vodacom Tanzania Public Limited Company (au ina program zinazosubiria). Bidhaa zingine na majina ya kampuni yaliyotajwa hapa yanaweza kuwa alama za biashara za wamiliki wao husika.

Matamko ya matarajio

Taarifa hii, ambayo inajumuisha matokeo ya Kundi la makampuni kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2024, ina ‘matamko ya matumaini’, ambayo hayajapitiwa au kuripotiwa na wakaguzi wa Kundi, kuhusiana na hali ya kifedha ya Kundi, matokeo ya uendeshaji na biashara na taarifa zinazohusiana na mipango na malengo ya Kundi la Vodacom. Hasa, matamko hayo ya kuangalia mbele yanajumuisha matamko yanayohusiana na: ufanisi wa baadaye wa Kundi la Vodacom; matumizi ya mtaji siku zijazo, ununuzi, kujitoa, gharama, mapato, masharti ya kifedha, sera ya gawio na maendeleo ya baadaye; mikakati ya biashara na uwekezaji inayohusiana na upanuzi na ukuaji wa Kundi la Vodacom; athari za udhibiti wa biashara za Kundi la Vodacom unaofanywa na serikali katika nchi inapofanya shughuli zake; matarajio ya Kundi la Vodacom kuhusiana na tarehe za uzinduzi na kuanza uuzaji wa bidhaa, huduma au teknolojia; matarajio kuhusu mazingira ya uendeshaji na hali ya soko; ongezeko la wateja na matumizi; na kiwango cha ongezeko la gawio kwa Kundi.

Matamko ya kuangalia mbele wakati mwingine, lakini si wakati wote, hubainishwa kwa matumizi yao ya tarehe katika wakati ujao au Maneno kama ‘nita’, ‘tarajia’, ‘kusudia’, ‘ninge’, ‘weza’, ‘paswa’, ‘amini’, ‘panga’ au ‘lenga’ (pamoja na miundo yao ya ukanushi).

Kwa hali yao, matamko ya kuangalia mbele kwa asili yanatabirika, yanaweza kukisiwa na yanajumuisha hatari na mashaka kwa sababu yanahusiana na matumio na yanategemea mazingira ambayo yanaweza kutokea au yasitokee siku za baadaye. Kuna sababu mbalimbali ambazo zinaweza kusababisha matokeo halisi na maendeleo kutofautiana kabisa kuanzia yale yaliyoelezwa au kumaanishwa na matamko haya ya kuangalia mbele. Sababu hizi ni pamoja na, ingawa hazishii hapo, zifuatazo: mabadiliko katika hali ya kiuchumi au kisiasa katika masoko yanayohudumiwa kwa shughuli za Kundi la Vodacom; ushindani mkubwa kuliko ilivyotarajiwa; gharama kubwa kuliko ilivyotarajiwa au matumizi ya mtaji; ongezeko dogo la wateja kuliko ilivyotarajiwa na kupungua kwa wateja wa kudumu; mabadiliko katika hali ya matumizi ya wateja wapya na waliopo; uwezo wa Kundi kupanua nafasi yake kimawanda au kuongeza muda au kuchukua leseni mpya; uwezo wa Kundi kufanikisha kuokoa gharama; uwezo wa Kundi kutekeleza mkakati wake wa kutumia mkongo; kuanza kutoa bidhaa na huduma mpya; huduma za data (mobile data), upanuzi wa Biashara na mtandao wa 4G, mabadiliko katika viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, na vilevile katika viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, na vilevile viwango vya riba; uwezo wa Kundi kupata faida kutokana na kuingia katika ubia au kufanya biashara pamoja na kuingia katika kufanya biashara ya huduma na utoaji wa leseni ya chapa; matokeo yasiyofaa kwa Kundi ya kufanya na kuchanganya ununuzi na utupaji; mabadiliko katika mfumo wa kisheria ambapo Kundi huendesha shughuli zake; athari za mashauri ya kisheria na mengineyo; kupoteza wasambazaji au kuvurugika kwa mnyororo wa usambazaji; maendeleo katika hali ya fedha ya Kundi, mapato na fedha zinazosambazwa na mambo mengine ambayo Bodi imezingatia wakati wa kuamua viwango vya magawio; uwezo wa Kundi kuwa na mtaji wa kufanyia kazi na mahitaji mengine; mabadiliko katika viwango vya kodi kisheria au mchanganyiko wa faida; na/au mabadiliko katika sharia ya kodi. Matamko mengine yote yaliyofuata ya kuangalia mbele yawe kwa maandishi au mdomo ambayo ni ya Kampuni, kwa mhusika yeyote wa Kundi au kwa watu wowote wanaofanya kwa niaba yao wanastahili katika wingi wao kwa sababu zinarejelewa hapo juu. Uhakika hauwezi kutolewa kuwa matamko ya kuangalia mbele katika waraka huu yatafikiwa. Kutegemea kufuata sharia na kanuni zinazotumika, Kampuni haikusudii kuboresha matamko haya ya kuangalia mbele na haichukui wajibu wowote wa kufanya hivyo.

